


UKURASA 5



**DK.** Mwinyi ataja mafanikio miaka miwili madarakani




UKURASA 9

**Nipashe** Jumapili Novemba 6, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581121
www.ippmedia.com
JUMAPILI
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# KIMENUKA

**BUNGE** latoa maazimio mazito, wakurugenzi, mawaziri wawekwa mtegoni... *Endelea ukurasa 2 na 3*



- SAKATA WABABA 731 KUJIFUNGUA
- KIBANO KIKALI MSD
- UFISADI BANDARI YA TANGA
- UKAGUZI MOTO KARIAKOO
- USIMAMIZI KIA CHINI YA TAA
- MIKOPO MATREKTA SUMA - JKT
- DENI LA SERIKALI TRIL. 1.5/- PSSSF
- UPIGAJI WAKUTISHA HALMASHAURI
- WAKOPAJI BENKI KUFILISIWA
- MIKATABA UNUNUZI TANESCO

Spika Dk. Tulia Ackson

## Afariki akiwa kwenye foleni kusubiri mbolea ya ruzuku




UKURASA 5

UKURASA WA 4

**RIPOTI MAALUM -2**

### MTIHANI WANANCHI WALIOSABABISHA MAJI YA BAHARI KUYAVAMIA MAKAZI



SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana ilikuwa na ushuhuda wa athari za mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira zinazowakumba wakazi...

UKURASA WA 8

### SHAKA AWATOLEA UVIVU WABADHIRIFU SERIKALINI

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, ametoa onyo na kuwatahadharisha...

**MICHEZO** YANGA SC YATUA KIBABE TUNISIA UK. 24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

# ‘Kimenuka’ bungeni

**Na Romana Mallya**



Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, akitoa ufafanuzi wa maswali yaliyoulizwa na baadhi ya wabunge, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

KIMENUKA! Ndicho ambacho wakazi wa mitaani wanaweza kutamka kutokana na kibano ambacho Bunge limekielekeza kwa watendaji wa serikali, wakiwamo mawaziri na wakurugenzi wa mashirika ya umma.

Wakati wa kuhitimisha hoja kuhusu taarifa ya utendaji wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), kamati hiyo iliwasilisha maazimio 14, yakigusa hoja nyeti zikiwamo za MSD kuwa na kiwango kikubwa cha dawa zilizokwisha muda wa matumizi na harufu ya ufisadi katika mradi wa Upanuzi wa Bandari ya Tanga.

Akisoma bungeni jijini Dodoma jana maazimio ya Bunge, Makamu Mwenyekiti wa PAC, Japhet Hasunga alisema yametolewa kwa kuzingatia matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), mahojiano na maofisa masuhuli na majadiliano na michango iliyotolewa tangu walipoanza kujadili taarifa ya kamati yao Novemba 2 mwaka huu.

Hasunga alisema azimio la kwanza linahusu nakisi ya ukusanyaji wa mapato ya serikali kupitia Mamlaka ya Mapato (TRA) Sh. trilioni 2.81, Bunge liazimie serikali ifanye mapitio ya kina ya mfumo mzima wa ukusanyaji wa kodi ili kuhakikisha fedha zote zinakusanywa kama ambavyo Bunge linaidhinisha kwa mujibu wa taratibu.

Hasunga alisema serikali ifanye uchunguzi na kuchukua hatua stahiki kwa watumishi wote wa TRA waliohusika katika kukadiria kodi chini ya kiwango, kutoshughulikia madeni ya kodi kwa wakati na kuchelewa kusajili mapingamizi ya kodi kwa wakati.

Kuhusu kutosimamia ushuru wa forodha kwenye bidhaa za mafuta na magari pamoja na usimamizi usioridhisha wa matumizi za mashine za kieletroniki (EFD), Hasunga alisema hali hiyo ilisababisha ongezeko la madeni ya kodi kwa zaidi ya asilimia 95 ndani ya mwaka huo wa fedha, hivyo kukosesha serikali mapato ya kuhudumia wananchi.

Azimio la pili linahusu dosari ya usimamizi wa mikataba na athari zake katika matumizi ya fedha za umma, Hasunga akisema kamati imebainisha upungufu katika uingiaji na usimamizi wake na kusababisha hasara kwa serikali ikiwamo Sh. bilioni 68.7 kwa TANROADS, TANESCO dola 153.43, NFRA dola 33.4 na TPA Sh. bilioni 137.38.

Kutokana na dosari hiyo, Hasunga alisema Bunge linaazimia serikali ifanye uchunguzi kubaini iwapo riba zilizotokana na mikataba ya ujenzi wa barabara (TANROADS) zilikuwa na uhalali na ulazima kuwapo.

"Hatua stahiki zichukuliwe kwa wahusika kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi huo, serikali ichukue hatua stahiki kwa watumishi wa Wizara ya Nishati, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Fedha na Mipango na TANESCO, walioshiriki katika mchakato mzima wa uingiaji, usimamizi, utekelezaji na uvunjaji wa mikataba kati ya TANESCO na Simbion.

"Serikali ichukue hatua stahiki za kisheria kwa mkandarasi aliyechelewesha kukamilisha ujenzi wa gati ya kuegesha meli katika Bandari ya Mtwara," Makamu Mwenyekiti huyo aliwasilisha maazimio ya Bunge.

Azimio la tatu ni kuhusu hali ya ukwasi katika taasisi za kimkakati za serikali; TPDC, TANESCO na STAMICO, Bunge likiazimia serikali kupitia ofisi ya Msajili wa Hazina iongeze mtaji katika mashirika ya kimkakati kwa kufanya marekebisho ya msingi katika madeni yake ili kuyageuza kuwa mtaji, pia ihakikishe mikataba inayoingiwa na mashirika hayo inakuwa na maslahi makubwa ya taifa.

Azimio la nne ni kuhusu ukaguzi maalum wa REA, Uhamiaji na Chuo cha Hombolo, Bunge likiazimia serikali ichukue hatua za kisheria kwa mkandarasi, Kampuni ya Derm Electrics Tanzania Ltd kwa udanganyifu na ubadhirifu pamoja na hatua za kisheria na kinidhamu kwa watumishi wa REA na TANESCO waliohusika kusimamia mradi wa REA awamu ya pili Mkoa wa Mara kwa kutokutimiza majukumu yao ipasavyo.

Hasunga alisema Bunge linaazimia serikali ichukue hatua za kisheria kwa watumishi 32 wa Jeshi la Uhamiaji waliotajwa kuhusika katika mauzo ya stika za visa bandia katika Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Kilimanjaro (KIA), kwa kuzingatia uhusika wa kila mmoja na matokeo ya ukaguzi maalum.

"Wakati wanakuja kwenye kamati, ni watumishi 11 tu walikuwa wamepelekwa mahakamani na hao wamesharejeshwa, hii ya kusema hatua zimeshachukuliwa, kama kamati mpaka juzi ilikuwa bado, labda waziri atatuambie kama zimechukuliwa," alisema.

Hasunga pia alisema serikali ichukue hatua za kisheria kwa watumishi wawili waliobainisha kujihusisha na ubadhirifu wa fedha za ada za wanafunzi katika chuo cha serikali za mitaa (Hombolo).

**SOKO KARIAKOO**

Azimio la tano ni kuhusu kutozingatiwa kwa sheria ya fedha za umma, Hasunga akisema Bunge linaazimia kuwa katika Shirika la Masoko Kariakoo, CAG afanye ukaguzi wa kiuchunguzi ili kubaini iwapo kuna ubadhirifu wa fedha za umma uliofanywa na kufichwa baada ya soko hilo kuungua.

"Pia vyombo vya dola vianze uchunguzi wa uliokuwa uongozi wa soko hilo ili kubaini iwapo wahusika wana jinai katika kuficha nyaraka za fedha kwa wakaguzi," alisema.

**DART**

Bunge pia liliazimia CAG afanye ukaguzi maalum wa malipo ya fidia Sh. bilioni moja na malipo ya fedha za usumbufu ya Sh. milioni 434 yaliyofanyika DART, ili kubaini iwapo yalifanyika kwa mujibu wa sheria.

"Mfuko wa Tozo na Tuzo wa Jeshi la Polisi, CAG afanye ukaguzi maalum wa matumizi yote ya mfuko tangu ulipoanzishwa na kisha kutoa taarifa yake kwa Bunge, mapema iwezekanavyo.

"Mlipaji Mkuu wa Serikali aandae kanuni za kusimamia uendeshaji wa mfuko huo na malipo yote kutoka kwenye mfuko yafanyike kwa kuzingatia kanuni zilizoandaliwa na mlipaji mkuu wa serikali," Hasunga alisema.

Azimio la sita ni kuhusu umiliki na uendeshaji wa Kampuni ya Uendeshaji wa KIA (CADIKO), Bunge likiazimia serikali irejeshe shughuli zote za uendeshaji kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kama ambavyo inafanyika kwa viwanja vingine nchini.

"CAG afanye ukaguzi wa kina wa mapato na matumizi ya CADIKO kuanzia mwaka 2010 baada ya kuanza kumilikiwa kwa asilimia 100 na serikali hadi sasa na Bunge lijulishwe ipasavyo.

Azimio la saba ni kuhusu utendaji wa kifedha wa benki za serikali; TCB na TID, Bunge likiazimia benki hizo zikusanye mikopo yote ikiwa ni pamoja na kutaifisha mali za dhamana zilizowekwa na wakopaji husika kwa mujibu wa sheria ili kurejesha mtaji wa benki hizo.

Pia vyombo vya dola vifanye uchunguzi wa mikopo yote chechefu iliyotolewa na benki hizo ili kubaini iwapo ilitolewa kwa kuzingatia taratibu za kibenki na kuchukua hatua dhidi ya watu waliohusika.

**BANDARI TANGA**

Azimio la nane ni kuhusu ubadhirifu katika upanuzi wa Bandari ya Tanga uliohusisha ubadhirifu wa Sh. bilioni 64.3, Bunge linaazimia serikali uchukue hatua za kisheria kwa kampuni na watumishi wote wa TPA waliotajwa katika taarifa ya ukaguzi maalum kuhusika kwao katika ubadhirifu wa fedha za umma wakati wa utekelezaji wa mradi huo.

Juzi Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Judith Kapinga, aliliibua bungeni sakata hilo, akitaka hatua zichukuliwe dhidi ya wahusika ili kuongeza uwajibikaji.

Azimio la tisa ni kuhusu kuharibika kwa dawa na kutokuwapo baadhi ya maeneo ya kutoa huduma za afya, Bunge likiazimia MSD wasitoe dawa, vitendanishi au chanjo ambazo muda wake wa matumizi upo chini ya miezi sita ya kutumika.

"Serikali isipokee dawa, vitendanishi au chanjo za msaada ambazo pia muda wake wa matumizi upo chini ya miezi sita. MSD ipeleke dawa kwa wakati kwa wanaohitaji kwa maeneo yote ambayo wamepokea fedha zao," Hasunga alisema.

Azimio la 10 ni kuhusu mapitio na tathmini ya hesabu za mifuko ya hifadhi ya Jamii, ripoti ya CAG ikibainisha kupungua kwa uwezo wa PSSSF kulipa mafao yake pamoja na uwapo wa deni ambalo mifuko PSSSF na NSSF inadai kwa serikali Sh. trilioni 1.5.

Hasunga alisema Bunge linaazimia serikali iwasilishe bungeni mpango wa malipo ya mikopo ya mifuko ya hifadhi ya jamii, kwa madeni yote ambayo mifuko inaidai serikali na mpango huo wa malipo uwasilishwe bungeni kabla ya kukamilika kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Azimio la 11 ni kuhusu upungufu katika uzingatiaji wa Sheria za Ununuzi wa Umma na kanuni zake, Bunge likiazimia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ichunguze ununuzi wenye dosari uliobainishwa na kamati katika taasisi za TANESCO fungu namba 57 na Wizara ya Ulinzi na kisha kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi.

"Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ianzishe uchunguzi kwa wahusika waliofanya ununuzi bila kuzingatia sheria katika taasisi hizo na kuchukua stahiki," Hasunga alisema.

Azimio la 12 ni kuhusu upungufu katika mifumo ya udhibiti wa ndani, Bunge likiazimia serikali ichukue hatua za kisheria kwa watendaji na kampuni zilizohusika na ununuzi na usimikaji wa mifumo ambayo imeshindwa kufanya kazi kwa ufanisi TPA.

**MATREKTA SUMAJKT**

Hasunga pia alisema Bunge linazimia Bodi ya SUMAJKT zichukue hatua za kinidhamu na za kisheria kwa watendaji waliokuwa wakisimamia mradi wa mauzo ya matrekta kwa kuruhusu uuzaji wake bila mikataba ya mauzo.

Azimio la 13 ni kuhusu taarifa ya ukaguzi wa ufanisi, Bunge likiazimia serikali iwasilishe bungeni taarifa ya mapendekezo ya ukaguzi na ufanisi yaliyotolewa na CAG kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB), Tume ya Madini, TANROADS na BRELA.

Hasunga alisema azimio la 14 linahusu usimamizi usioridhisha wa taarifa na huduma katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na kuwapo kwa dosari ya utoaji huduma ikiwamo utolewaji wa huduma za uzazi wa upasuaji kwa wanaume 731.

Pia kukataa kulipa malipo ya Sh. bilioni 3.18 kwa hospitali za serikali zilizotoa huduma kutokana na kuwa na mfumo wenye upungufu na utambuzi na usimamizi wa taarifa.

Hasunga alisema Bunge linaazimia serikali ifanye uchunguzi wa idara ya usimamizi na udhibiti wa huduma NHIF ili kubaini iwapo inatekeleza majukumu yake ipasavyo.

# MAAZIMIO YA BUNGE



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama (katikati), akimsikiliza Mbunge wa Babati Vijijini, Daniel Sillo (kulia) na Mbunge wa Nkasi,Vicent Mbogo, walipokutana katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# ...wakurugenzi wawekwa mtegoni

**Na Richard Makore,** DODOMA

WAKATI hali ikiwa hivyo katika maazimio kuhusu taarifa ya PAC, Bunge pia limetoa maazimio kuhusu hoja zilizoibuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC) ili kuhakikisha kunakuwa na uwajibikaji na kudhibiti mapato ya serikali.

Makamu Mwenyekiti wa LAAC, Stanslaus Mabula alisoma bungeni jana maazimio ya Bunge kuhusu taarifa ya kamati yake, akibainisha kuwa katika kuhakikisha kunakuwa na uwajibikaji kwa watumishi wa umma, Bunge linaazimia serikali kuchukua hatua kwa watumishi wa halmashauri walioshindwa kusimamia fedha za mikopo kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Katika kudhibiti fedha za serikali, Mabula alisema Bunge linaazimia halmashauri zote kupewa ruzuku sawa inayotolewa na serikali pamoja na halmashauri kutorejesha serikalini fedha za miradi ambazo muda unaisha kabla hazijatumika.

Mabula alisema Bunge pia linaazimia serikali kuhakikisha halmashauri zinazingatia suala la uwekezaji katika miradi mingine badala ya kuendelea kujikita kuwekeza katika masoko na vituo vya mabasi.

Kuhusu ununuzi wa umma, Mabula alisema Bunge linaazimia serikali kusimamia ununuzi wote wa serikali kwa idhini ya Bunge.

Kuhusu uwajibikaji katika ulipaji wa ujira na stahiki za watumishi, Makamu Mwenyekiti wa LAAC alisema Bunge linaazimia kuchukuliwa hatua waajiri wanaominya stahiki za watumishi wao.

Katika kudhibiti mapato ya serikali, Bunge liliazimia watendaji wa serikali wanaokusanya mapato bila kufuata utaratibu wachukuliwe hatua.

Azimio lingine la Bunge ni kuhakikisha fedha za amana zilizowekwa katika benki za serikali zitumike kwa uwazi.

Bunge pia liliazimia serikali kuwachukulia hatua watumishi wake wanaosababisha upotevu wa mapato.

Azimio la tisa Bunge kuhusu taarifa hiyo ya LAAC ni kudhibiti hasara ikiwamo kuhakikisha Bohari ya Dawa (MSD) kutopeleka dawa katika vituo vya afya na hospitali wakati muda wake wa kutumika ukiwa unakaribia kuisha.

Kuhusu wakala wa ununuzi wa serikali, Bunge liliazimia halmashauri zisipokee dawa zinazokaribia kumaliza muda wake.

Bunge pia liliazimia serikali kuhakikisha inapeleka watumishi wenye sifa za kielimu katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utendaji ndani ya serikali.

**TAARIFA YA PIC**

Bunge pia lilitoka na maazimio kuhusu taarifa ya utendaji wa PIC, yakisomwa bungeni na Mwenyekiti wake, Jery Silaa, akianza na azimio la kuitaka serikal kuhakikisha inafanya uteuzi wa wenyeviti wa bodi katika taasisi na mashirika mbalimbali ya umma ili yawe na usimamizi kiutendaji.

Bunge pia liliazimia mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara, yapewe vibali vya kuajiri watumishi wake.

Silaa pia alisema Bunge linaazimia Mamlaka ya Bandari (TPA) kuboresha Bandari za Dar es Salaam na Bagamoyo ili kusaidia usafirishaji wa bidhaa kupitia reli ya kisasa itakapokamilika.

Vilevile, Bunge liliazimia serikali ihakikishe inakamilisha mazungumzo ya mwisho ili kukamilisha miradi ya Liganga na Mchuchuma.

Silaa alisema Bunge pia linaazimia serikali kufanya tathmini ya mikopo katika benki zake pamoja na Wakala wa Ndege za Serikali kurudisha ndege zake kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL).

Kuhusu hali mbaya ya mitaji ya baadhi ya benki za umma, Silaa alisema Bunge linaazimia kuipatia mtaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), serikali kulipa deni la Sh. bilioni 21 za wafanyabiashara wa pamba ilizoahidi kulipa kama ruzuku kwa wafanyabiashara walionunua pamba za wakulima.

Bunge pia liliazimia serikali kurudisha jukumu la ujenzi wa viwanja vya ndege kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Viwanja vya Ndege (TAA) badala ya kusimamiwa na Wakala wa Barabara (TANROADS).

Silaa pia alisema Bunge linaazimia serikali kukamilisha mifumo ya TEHAMA kudhibiti udanganyifu, Mamlaka ya Bandari (TPA) kurudisha mali za MSC ikiwamo cherezo na karakana.

Bunge pia liliazimia serikali ihakikishe inasimamia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kuwa na mfumo wa TEHAMA ili kudhibiti udanganyifu.

Agizo lingine ni pamoja na kuangalia namna kupata unafuu katika ukataji wa bima kwa ndege za serikali kwa kuwa hivi sasa gharama za bima ni kubwa, zikisimamiwa na Shirika la Bima la Taifa kwa kutegemea mkataji wa bima kutoka nje ya nchi.

Kabla ya kutolewa maagizo hayo, baadhi ya mawaziri walipewa fursa ya kuchangia katika hoja zilizowasilishwa na kamati hizo zilizofanya uchambuzi wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Miongoni mwa mawaziri hao ni wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa aliyesema Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) unamilikiwa na serikali kwa asilimia 100.

# Majaliwa atoa angalizo ugawaji wa vishikwambi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetoa maagizo tisa ya ugawaji na matumizi ya vishikwambi 293,400 vilivyogawiwa kwa walimu nchini huku ikionya matumizi yasiyo sahihi ya vifaa hivyo.

Vishikwambi hivyo ni kati ya 300,000 vilivyotumika kwenye sensa ya watu na makazi mwaka huu ambapo Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza baada ya kukamilisha kazi ya sensa, vigawiwe kwa walimu ili kuimarisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alielekeza hayo jana jijini hapa kwenye hafla ya uzinduzi wa ugawaji wa vifaa hivyo kwa sekta ya elimu nchini.

Alisema serikali imedhamiria kuwekeza kwenye Tehama hivyo vishikwambi viwafikie walengwa waliokusudiwa ili kuleta mapinduzi ya elimu nchini ikiwa ni utekelezaji wa Sheria ya Tehama ya Mwaka 2016.

"Ninataka vifaa hivi viwafikie walengwa wote kwa wakati ili waweze kufanya kazi, hapa ningependa kusisitiza kwamba vifaa hivi ni kwa walimu tu na kweli viwafikie na kutumika na walimu na si vinginevyo," aliagiza.

Majaliwa alisema kishikwambi hicho kitakuwa ni mali ya mwalimu husika na atakayekosa, apeleke taarifa kwa wizara inayohusika ili ifuatilie.

"Tunaamini kuwapo vifaa hivi kutahamasisha sana matumizi ya teknolojia katika ufundishaji, kwa kutumia wataalamu wa ndani wa kila halmashauri uandaliwe utaratibu wa kutoa mafunzo ya msingi ya matumizi ya vifaa hivi, katika ngazi ya kata na wilaya," alisema.

Alisisitiza walimu wote kutunza vifaa hivyo na kuvitumia kwa malengo kusudiwa ya elimu ikiwamo katika kufundishia somo la Tehama na kwa kurahisisha ufundishaji.

"Vitumike katika kuondoa changamoto ya zana mbalimbali za kufundishia na kujifundishia vifaa rejea kwa walimu, itumike kama nyenzo ya kuwezesha walimu kufikia zana mbalimbali za kuwezesha tendo la ufundishaji na ujifunzaji ikiwamo maktaba mtandao, maktaba ya Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE), iliyo na vitabu mbalimbali vya kiada, ziada na miongozo mbalimbali ya kufundishia video na masomo yaliyoandaliwa kwa sauti," alisema.

Waziri Mkuu alitaka walimu watumie mafunzo mbalimbali wanayoyaleta kwenye mtandao wa mafunzo endelevu kazini kwa walimu inayojulikana kwa jina la MEWAKA yawakute wakiwa shuleni.

Awali, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof.Adolf Mkenda alisema "Vishikwambi 300,000 vilinunuliwa kwa ajili ya sensa na kwamba baadhi ya vishikwambi vilipelekwa Ofisi ya Takwimu kwa ajili ya sensa ambapo Zanzibar vilipelekwa 6600 na 293,400 vilibaki Tanzania Bara."

Alifafanua mgawanyo wa vishikwambi hivyo kuwa ni walimu wa shule za msingi za umma 185,404, walimu wa shule za sekondari 89,805, Wathibiti Ubora wa Shule ngazi ya Wilaya na Kanda 1,666, Wakufunzi wa vyuo vya ualimu vya umma 1,393, wakufunzi wa vyuo vya maendeleo ya wananchi 267, Maofisa Elimu Mikoa, Wilaya na Kata 5,772.

Pia alisema kwa wakufunzi wa vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (VETA) vishikwambi 996 na Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA) vishikwambi 8,357.

Alitaja faida mbalimbali za matumizi ya vishikwambi hivyo kuwa ni kupunguza gharama na matumizi ya karatasi, kusafiri na kurahisisha upatikanaji wa vyenzo za kujifunzia na kufundishia na usahihishaji wa mitihani.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**

**MAHAKAMA YA MWANZO KEREGE WILAYA YA BAGAMOYO**

**MADAI NAMBA 24 LA 2022**

**Mdai CHRISTINA SUSA**

**Mdaiwa ISSA GWANDAJA**

**KWA: ISSA GWANDAJA – MKULAZI – MOROGORO**

**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba**

**KUJA KUJIBU MADAI (1) TALAKA (2) MATUNZO YA WATOTO NA (3) MGAO WA MALI ZA NDOA**

Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya IJUMAA ya tarehe 11/11/2022 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukata shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama mmepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo IJUMAA ya tarehe 4 Mwezi wa 11 mwaka 2022.

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO KEREGE - BAGAMOYO



**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**

**MAHALI DODOMA, LILILOKO DODOMA**

**MAOMBI MADOGO NA. 425 YA mwaka 2022**

**CYNOCK LYIMO............................... MKAZA HUKUMU**

**VERSUS**

**SELEMANI JUMA HASSAN ................ MKAZIWA HUKUMU**

**KWA: SELEMANI JUMA HASSAN**

**POPOTE ULIPO**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 10.11.2022 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANAGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 03 ya mwezi wa Novemba, 2022.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

RIPOTI MAALUM -2

# Mtihani wananchi waliosababisha maji ya bahari kuyavamia makazi

Na Mary Geofrey, aliyekuwa
MTWARA

## ■Serikali yaanika mikakati kukabili athari

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana ilikuwa na ushuhuda wa athari za mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira zinazowakumba wakazi wa Mikindani mjini Mtwara, zikijumuisha maji ya bahari kuvamia makazi yao. Endelea na sehemu ya mwisho kujua hatua zaidi zinazochukuliwa.**



Mkazi wa mtaa wa Kisungule A, Mikindani mkoani Mtwara, Moza Ahma, akionyesha namna wanavyotumia taka kuzuia maji ya bahari kuingia kwenye makazi yao. **PICHA: MARY GEOFREY**

OFISA Mazingira Halmashauri ya Minispaa ya Mtwara Mikindani, Tumaini Mosha anabainisha wamejiwekea utaratibu wa kuotesha miti 16,000 kila mwaka katika maeneo mbalimbali wakati wa msimu wa mvua ili kudhibiti athari za mabadiliko ya tabianchi.

Kuhusu tatizo la uchimbaji wa mchanga katika eneo hilo, ofisa huyo alisema unafanyika kinyume cha Sheria ya Madini inayowataka wanaofanya kazi hiyo kuwa na leseni.

"Hatujapata malalamiko ya uchimbaji wa mchanga eneo hilo. Wanaofanya hivyo, wanavunja sheria, hivyo tukiwabaini tutawachukulia hatua kwa mujibu wa sheria," anaonya.

### HATUA ZA MKOA

Ofisa Maliasili na Mazingira Mkoa wa Mtwara, Ronald Panga, anabainisha misitu inayopatikana eneo la bahari pekee ni hekta 14,000 na kwa Mkoa wa Mtwara inapatikana katika vijiji vitano, ikiwa ni pamoja na Mikindani.

Anasema misitu ya mikoko inatumika kuzuia mmomonyoko wa udongo, chakula cha viumbe wakiwamo samaki na kuhifadhi bahari, akiyataja maeneo makuu yaliyoathiriwa na shughuli za ukataji wa mikoko kuwa ni Mikindani na Shangani.

Panga anasema kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Na. 14 ya Mwaka 2002, hairuhusiwi mtu yeyote kukata miti ya msitu bila kibali maalum, hivyo waliokuwa wanakata mikoko walifanya uvunjaji haramu.

Anasema shughuli hizo zilifanyika usiku kwa sababu wanajua ni kosa na kazi kubwa, akibainisha kuwa miti hiyo ilitumika kama fito za kujengea nyumba na kuni za kuchomea matumbawe.

Ofisa huyo anataja hatua walizozichukua kudhibiti uharibifu huo ni kutoa elimu ya umuhimu wa misitu hiyo, njia mbadala ya kututumia kujengea badala ya miti na athari za ukataji miti, yakiwamo mabadiliko ya tabianchi.

Anasema moja ya athari za ukataji wa miti hiyo ni kupwa na kujaa kwa bahari na maji kuingia kwenye makazi ya watu.

Panga anasema eneo la Mikindani limeathiriwa zaidi kwa kuwa nyumba zake nyingi zipo ndani ya mita 60 kutoka baharini kinyume cha Sheria ya Mazingira.

"Wengi wa wakazi wa Mikindani wapo ndani ya maji, wengine mita 10, wengine mita tano kinyume cha sheria," anabanisha.

Panga anasema Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wanazuia shughuli hizo na kutoa elimu kwa jamii na kueleza faida za misitu hiyo.

Ofisa huyo pia anabainisha kuwa katika eneo la Mikindani wanatekeleza mradi wa kuongeza fukwe na kuzuia mmonyoko wa udongo kwa kushirikiana na wananchi wa eneo hilo.

Panga pia anakiri kuwapo shughuli za uchimbaji mchanga kufuatia malalamiko aliyopokea kutoka kwa wadau wa maendeleo katika eneo hilo, akiahi kufanyia kazi kwa kushirikiana na uongozi wa halmashauri hiyo.

Anasema wanaendesha kampeni ya kuotesha mikoko katika maeneo ambako imekatwa ili kurejesha hali ya zamani.

### KAULI YA NEMC

Meneja wa Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Mkoa wa Mtwara, Boniphace Guni, anasema hana taarifa ya shughuli ya uchimbaji mchanga katika eneo hilo, akisisitiza ni kinyume cha sheria.

Guni anaahidi kufuatilia taarifa hiyo aliyoipokea kutoka Nipashe na baadaye kutoa taarifa kuhusu suala hilo.

Nipashe pia inatua mezani kwa Ofisa wa Mkazi Wizara ya Madini Mkoa wa Mtwara, Ephraim Mushi ambaye anasita kutoa taarifa kuhusu tatizo la uchimbaji mchanga katika eneo la Mikindani, akisisitiza ni sharti apate kibali kutoka ngazi ya juu ya wizara hiyo.

Kwa mujibu wa takwimu za Mkoa wa Mtwara, kwa sasa mkoa huo una leseni 386, leseni 17 za utafiti, leseni moja ya uchimbaji mkubwa, leseni nne za uchimbaji wa kati na leseni 364 za uchimbaji mdogo.

### MIKOKO KITAIFA

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii (1991 na 2015), kumekuwapo na kupungua kwa mikoko katika ukanda ya kaskazini na kusini kutoka hekta 11,159 hadi 1,701 na kutoka hekta 35,159 hadi 30,981 katika mwaka 1991 hadi 2015 mtawalia.

Hata hivyo, taarifa hiyo inabainisha kumekuwapo na ongezeko la mikoko kutoka hekta 68,390 mwaka 1991 hadi hekta 125,418 mwaka 2015 katika Kanda ya Kati inayojumuisha mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Juni mwaka huu ilizindua Mpango Kabambe wa Taifa wa Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira.

Lengo Kuu la Mpango Kabambe huo ni kutoa mwongozo wa hatua za kuchukuliwa kutatua shida za mazingira nchini kwa kuzingatia sehemu husika na hatua mahsusi zinazopaswa kuchukuliwa.

Malengo mahsusi ya Mpango Kabambe ni kuainisha hali ilivyo ya shida za mazingira ikiwamo visababishi, athari zake, hatua zilizoendelea kuchukuliwa na vikwazo.

Vilevile, kutoa mwelekeo wa kimkakati wa mabadiliko yanayohitajika kuleta matokeo chanya, kuainisha maeneo ya vipaumbele na kuainisha hatua mahsusi zinazopaswa kuchukuliwa ili kukabiliana na shida za mazingira husika.

Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC) na ni miongoni mwa nchi zilizowasilisha mchango wake wa kukabiliana na athari hizo katika Sekretarieti ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi Julai 30 mwaka jana.

## Wahamiaji haramu wafa kwa ajali wakienda 'Sauzi'

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

RAIA wawili wa Ethiopia wamefariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa huku wanne wakitoroka baada ya gari walilokuwa wakisafiria kupelekwa Afrika Kusini kuacha njia na kupinduka.

Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Singida, Phaustine Ngunge, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 26 mwaka huu katika Kijiji cha Mitundu wilayani Manyoni mkoani hapa.

Alisema wahamiaji hao haramu ambao jumla walikuwa tisa walikuwa wakisafirishwa katika gari aina ya Toyota Land Cruiser ambalo namba za usajili hazijajulikana, akibainisha majeruhi walipelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Manyoni kwa matibabu.

Ngunge alisema wahamiaji wanne ambao hawakujeruhiwa katika ajali hiyo, walikimbia na kwenda kusikojulikana lakini baada ya siku moja walijisalimisha katika Kituo cha Polisi Mitundu wilayani Manyoni.

Alisema waliofariki dunia katika ajali hiyo, miili yao imehifadhiwa katika Hospitali ya Mkoa wa Singida ambapo taratibu za mazishi zifanyika baada ya kupata kibali kutoka Ubalozi wa Ethiopia ama kuzikwa nchini au kusafirishwa.

Kuhusu majeruhi, alisema wametibiwa na kupona na kwamba hadi sasa wanashikiliwa na Jeshi la Uhamiaji ambapo kesho watuhumiwa saba wanatarajia kufikishwa mahakamani kujibu tuhuma za kuingia nchini bila kuwa na kibali.

Aliongeza kuwa dereva wa gari lililowasafirisha, ametoroka na hajulikani aliko na gari hilo lililotumika kuwasafirisha wahamiaji hao haramu linashikiliwa katika Kituo cha Polisi Mitundu.

Ofisa huyo wa Uhamiaji alisema katika mahojiano na wahamiaji hao, walisema wametumia miezi minane kutoka Ethiopia hadi kufika mkoani Singida.

Kufuatia tukio hilo, Ngunge alionya Watanzania wakiwamo askari kutojiingiza katika biashara ya kusafirisha wahamiaji haramu kwa kuwa wakikamatwa, watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

"Ninatoa wito kwa wananchi wa Mkoa wa Singida mnapomtilia shaka mtu ambaye siyo raia wa Tanzania, mtoe taarifa katika Jeshi la Uhamiaji na katika chombo chochote cha usalama," alisema.

Tukio hili limekuja siku chache baada ya askari mkoani Mbeya kukamatwa wakituhumiwa kusafirisha wahamiaji haramu.

# Afa kwenye foleni mbolea ruzuku

**Na Waandishi Wetu**

MKULIMA Florence Nyingo (40), mkazi wa Kijiji cha Nakahuga, Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma, anadaiwa kufariki dunia muda mfupi baada ya kuanguka akiwa kwenye foleni ya kununua mbolea ya ruzuku.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Marko Chilya alisema tukio hilo lilitokea Alhamis jioni kwenye eneo la ghala la kuhifadhi mbolea ya ruzuku.

Alisema ghala hilo liko karibu na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Ruvuma, akifafanua kuwa mkulima huyo, akiwa kwenye foleni, alianguka na kukimbizwa hospitalini huko ambako madaktari walithibitisha kifo chake.

Kamanda huyo alisema mkulima huyo alikuwa ametokea Kijiji cha Nakahuga, Songea Vijijini na alifika huko kwa ajili ya kutafuta mbolea ya ruzuku na kwamba eneo la tukio kulikuwa na foleni ndefu ya wahitaji wa mbolea hiyo.

**SAKATA BUNGENI**

Jana wakati wa majadiliano ya ripoti za utendaji wa kamati za kudumu za Bunge jijini Dodoma, Mbunge wa Viti Maalum, Kunti Majala aliliibua suala hilo.

Mbunge huyo alisema fedha nyingi za serikali za miradi zinapotea kutokana na wizi pamoja na kuingia mikataba mibaya, akisisitiza zingesaidia wakulima kupata mbolea.

Alisema mkulima aliyefariki dunia akiwa katika foleni ni kielelezo kuwa kuna shida ya mbolea kwa wakulima.

"Wakulima hawana mbolea mpaka mtu anafia katika foleni akisubiri mbolea ya ruzuku, wakati kuna watumishi ndani ya serikali wanaiba fedha za umma katika miradi mbalimbali," alisema.

Wakati mbunge huyo akiendelea kuchangia, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel alisimama na kumpa taarifa kuwa mtu hawezi kufariki dunia kwa kuwa yupo katika foleni na kwamba hakuna uthibitisho huo.

Dk. Mollel alisema hiyo siyo sababu ya chanzo cha kifo kitaalamu na kuomba mchangiaji afute kauli yake ili aendelee kuchangia hoja.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Eliezer Feleshi alisimama na kumpa taarifa mchangiaji kuwa mkulima huyo hakufariki dunia kutokana na foleni ya kusubiri mbolea.

Hata hivyo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson aliingilia kati sakata hilo na kusema taarifa hizo mbili hazikuwa na uzito kwa Mbunge Kunti.

Spika alisema suala mtu kufariki dunia akiwa katika foleni kama lilitokea halina ubishi kwa sababu ni kweli alifariki dunia akiwa eneo hilo.

■**Imeandaliwa na Gideon Mwakanosya (SONGEA) na Richard Makore (DODOMA)**



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na kujibu maswali wakati wa mkutano wake na wahariri na waandishi wa habari, Ikulu, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Mwinyi aanika mafanikio ya miaka miwili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema licha ya changamoto ya UVIKO-19 na vita vya Russia na Ukraine, ndani ya uongozi wake wa miaka miwili ukusanyaji wa mapato umeongezeka katika serikali yake.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu, Zanzibar wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya miaka miwili ya uongozi wake tangu alipochaguliwa mwaka 2020.

Alisema ongezeko hilo la mapato linatokana na idadi kubwa ya watalii wanaofika Zanzibar. Alisema hali hiyo imeanza kurejea kama ilivyokuwa kabla ya janga la UVIKO-19.

Rais alisema anajivunia uchumi kuimarika licha ya janga la UVIKO-19 na vita vya Ukraine na Russia vinavyoikumba dunia na kusababisha uchumi kusimama na sasa kuna kila dalili hali ya uchumi kurejea katika hali yake ya nyuma na kuvuka malengo.

Alisema katika sekta ya utalii wageni wameongezeka na kwa mara ya kwanza Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume umekuwa namba moja kwa kuingiza watalii wengi na kuakisi mapato yanayopatikana kutokana na uingiaji wa wageni.

"Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wakati naingia madarakani walikuwa wanategemea mishahara kutoka serikali na serikali ikitoa Sh. milioni 400 kila mwezi kwa ajili ya kulipa mishahara. Nafurahi kusema katika kipindi cha miezi mitatu, robo ya kwanza ya Julai hadi Septemba, mwaka huu, wamevunja rekodi ya mapato kwa kuingiza Sh. bilioni 6.7," alisema.

Dk. Mwinyi alisema kuna kila sababu ya kujivunia mipango ya kukusanya mapato vizuri ili kuleta maendeleo. Alisema ukusanyaji wa fedha ni mzuri katika serikali yake na imetokana na hatua zilizowekwa ikiwemo mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kielektroniki.

Kwa mujibu wa Dk. Mwinyi, ndani ya miaka miwili ya uongozi wake, pia amefanikiwa kutekeleza maridhiano ya kisiasa ambayo yamefungua milango ya uwekezaji na ukuaji wa uchumi katika sekta mbalimbali.

Alisema maridhiano hayo yanatokana na hali ya amani na usalama lakini pia ushirikiano kati ya viongozi wakiwamo wanasiasa na wananchi.

Mafanikio mengine, alisema ni kuongezeka kwa uwekezaji na miradi iliyosajiliwa ndani ya miaka miwili ni 181 yenye thamani ya dola bilioni tatu.

Miradi hiyo itazalisha ajira 11,289 na kituo cha uwekezaji Zanzibar (ZIPA) imeimarisha huduma zao na cheti cha uwekezaji sasa kinatolewa ndani ya muda wa maa 24 endapo mwekezaji atatimiza masharti yanayotakiwa.

Alisema hatua hiyo itaendeleza kukuza uchumi wa nchi kwa sababu uchumi unategemea fedha za wawekezaji kutoka nje.

Kuhusu miradi ya maendeleo alisema hospitali za wilaya 10 zinaendelea kujengwa, ujenzi wa shule za gorofa, miradi ya maji na barabara ambapo ikikamilika huduma zitakuwa bora.

Alisema serikali yake imesimamia suala la utawala bora ikiwemo kutoa hadharani ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na hatua kuchukuliwa kwa wale wote waliotajwa katika ripoti hiyo kuhusika na ubadhilifu wa umma.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu iliyobaki miradi mikubwa inatarajiwa kutekelezwa ili kubadilisha uchumi wa Zanzibar ikiwemo ujenzi wa bandari ya Mangapwani, ujenzi wa barabara kuu ikiwemo ya Kisauni-Fumba, ujenzi wa barabara za ndani zenye kilomita 200 na ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali inapaswa kuzingatia ushauri kuhusu mikataba nyeti

**KWA** miaka mingi, serikali kupitia wizara zake za kisekta, imekuwa ikiingia mikataba mbalimbali na taasisi za ndani au za nje kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Miongoni mwa miradi hiyo ni ya uchimbaji wa madini na mafuta ambayo hugharimu mabilioni ya shilingi.

Mikataba hiyo imekuwa ikilalamikiwa mara kwa mara na wadau wakiwamo Wabunge kutokana na upungufu unaojitokeza ikiwamo baadhi ya watu wanaoiwakilisha serikali wakikosa umakini au kuegemea kwenye maslahi binafsi. Kutokana na kuwapo kwa mazingira hayo, mikataba mingi imekuwa ikisababisha serikali kuingia hasara au kutekelezwa kwa kiwango duni huku nchi ikiwa hainufaiki kama inavyopasa.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, katika mkutano wa Bunge unaoendelea jijini Dodoma, Mbunge wa Masasi (CCM), Geoffrey Mwambe, ameshauri serikali kupeleka bungeni mikataba yote ya miradi mbalimbali inayoingia ambayo inazidi Sh. bilioni tano ili ijadiliwe kutokana na taifa kupata hasara inapovunjika kutokana na kulipwa fedha nyingi. Akichangia hoja kwenye ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) zilizowasilishwa bungeni na Kamati za Kudumu za Bunge za Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Serikali (PAC) na Mitaji na Uwekezaji (PIC). Mwambe alisema serikali inashindwa kesi nyingi katika mikataba iliyowahi kuingia.

Mbunge huyo ambaye kitaaluma ni mchumi, aliweka bayana kuwa serikali imeshindwa katika mashauri mbalimbali yatokanayo na mikataba isipokuwa mmoja tu wa City Water. Kampuni hiyo iliingia mkataba wa kutoa huduma za maji kwa niaba ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) lakini ilishindwa kukidhi kiu ya wananchi ya kupata maji kwa uhakika.

Kutokana na ukweli huo, Mwambe alisema mikataba hiyo inaliangamiza taifa letu, hivyo imefika wakati sasa iwe inawasilishwa bungeni na kujadiliwa. Kwa kufanya hivyo, kwa mujibu wa mbunge huyo, wabunge watapata nafasi ya kuipitia na kutoa maoni yao kwa niaba ya wananchi kabla ya kutiwa saini rasmi kwa utekelezaji. Mwakilishio huo wa wananchi alikwenda mbali zaidi na kupendekeza hata mikataba ya zamani ambayo serikali ilishaingia na kampuni au taasisi za nje na za ndani, iwasilishwe bungeni kwa kudurusiwa ili kuangaliwa kama imezingatia maslahi ya taifa.


Alitolea mfano wa mkataba wa ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere katika Mto Rufiji kuwa umesogezwa kinyemela kwa miaka miwili, jambo ambalo ni hasara kwa taifa. Kwa kusogezwa mkataba huo, maana yake uzalishaji wa umeme utacheleweshwa hatua ambayo itawasababishia wananchi kukosa umeme kwa wakati kama walivyotarajia. Ushauri uliotolewa na mbunge huyo unapaswa kuzingatiwa na serikali kwa sababu ya maslahi mapana ya taifa. Kama alivyosema iko mikataba mingi ambayo imelitesa taifa kiasi cha kuifanya nchi kushindwa kupiga hatua kimaendeleo.

Mfano wa mikataba ambayo imelisumbua taifa ni ule wa kufua umeme baina ya serikali na Independent Power Tanzania Limited (IPTL). Mkataba huu umesababisha utata mkubwa kimaudhui hata utekelezaji wake na matokeo yake wananchi ndio wamekuwa wanaumia kwa kulipa gharama kubwa za umeme.

Mikataba kama hiyo, inapaswa kuangaliwa kwa makini katika mchakato mzima kuanzia kutafuta wabia au makandarasi wa utekelezaji wa miradi. Kwa kufanya hivyo, kutaiwezesha serikali kujua kama kampuni husika ina uwezo na inajulikana badala ya kutegemea taarifa zo mitandao na zisizothibitishwa.

Uhalisia katika hili ni sakata la kampuni ya Richmond Development Corporation LLC, iliyopewa zabuni ya kufua umeme iliyodaiwa kuwa ni ya Marekani lakini uchunguzi ulipofanyika ilibainika haijawahi hata kufunga balbu ya umeme. Matokeo ya mkataba huo ulisababisha viongozi waandamizi serikalini kuachia ngazi na kuvunjwa baraza la mawaziri. Kwa mantiki hiyo, ushauri kwa serikali kuwasilisha mikataba minene bungeni ili ijadiliwe kabla ya kutiwa saini kwa ajili ya utekelezaji ni muhimu na serikali inapaswa kuzingatia ili kuepusha hasara na matatizo yanayoweza kujitokeza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kwa mfumo huu, mikopo ya halmashauri sasa mwiba kwa wajanja

**OFISI** ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) , imekuja na mfumo mpya wa kielektroniki, utakaotumika kutoa mikopo ya asilimia 10 ambayo ni makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa makundi matatu.

Makundi hayo ni ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ambapo vikundi vinatakiwa kujisajili na kutuma maombi kwa njia ya mtandao, lengo likiwa ni kuongeza uwazi wa uombaji, utoaji na urejeshaji wa mikopo hiyo.

Inaelezwa kuwa mfumo huo pia utasaidia kuongeza uwajibikaji, usawa na uadilifu katika kutoa huduma ya mikopo kwa vikundi husika na kuvisaidia kuwa na takwimu sahihi na kurahisisha utoaji wa mikopo kwa wakati

Aidha, kupitia mfumo huu itatusaidia sana kuhakikisha kwamba waombaji wanapata mikopo kwa uwazi lakini pia kuhakikisha zile fedha zinazokopeshwa zinakuwa rahisi kurejeshwa kwa wakati.

Hayo ni kwa mujibu wa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, wakati akihojiwa na vyombo vya habari kuhusu uanzishwaji wa mfumo huo hivi karibuni.

Kwa mfumo huo mpya wa utoaji mikopo ya halmashauri, ninaamini kwamba utakuwa mwiba kwa wajanja wachache ambao wamekuwa wakiitumia kinyume na makusudi au kutoirejesha kwa wakati.

Hiyo inatokana na kwamba, baada ya kupata hati ya usajili ambayo inapatikana pia kwa njia ya kielektroniki, kikundi kinaweza kuomba mkopo kwa kuwasilisha maombi kwa njia ya mfumo na kupitishwa na kamati mbalimbali za mikopo kwa kuzingatia vigezo vyote.

Jambo la kwanza linalotakiwa kufanywa kupitia mfumo huo, ni kusajili kikundi kwa kutengeneza akaunti na kuweka taarifa sahihi, na kwamba kama taarifa zote zitakuwa sahihi mfumo utamtumtumia mhusika barua pepe.

Ujumbe huo pia unaweza kuwa kwenye namba ya simu kwa ajili ya uhakiki na baada ya hapo mhusika ataweza kuingia ndani ya mfumo, ili kumalizia kujaza taarifa mbalimbali za kikundi zikiwamo za wanakikundi.

Mbali na hayo, inaelezwa kuwa taarifa zao zitaambatana na viambatisho mbalimbali ikiwamo katiba na kisha kuziwasilisha taarifa za kikundi kwenye mfumo kwa ajili ya kupata hati ya usajili.

Kwa uwazi kama huo, wale ambao walikuwa wamezoea kuwa na vikundi hewa au watendaji waliokuwa wanatumia mwanya huo kuunda vikundi hewa kwa ajili kujinufaisha, huo ndio mwisho wao.

Utaratibu wa zamani wa utoaji mikopo umekuwa ikigubikwa na malalamiko ikiwamo baadhi ya waombaji kudai kunyimwa na watendaji wa halmshauri na baadhi ya wakopaji kutorejesha mkopo kwa wakati.

Vilevile kumekuwapo na vikundi hewa, hali ambayo husababisha fedha nyingi za halmshauri kuishia mikononi mwa wajanja wachache huku wengine wanaosubiri mikopo hiyo irejeshwe ili nao wakope wakiishia kuikosa.

Itoshe kusema tu kwamba, asante serikali kwa kuja na mfumo huo ambao ninaona kama mkombozi kwa wakopaji wenye nia njema waliokuwa wakiikosa kutokana na kuwapo wajanja wachache wanaoitumia kinyume.

Ikumbukwe kuwa fedha za mkopo zinazotolewa na halmashauri kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, kwa ajili ya kutumika kwenye miradi iliyokusudiwa ili kuinua uchumi wa vikundi hivyo.

Hivyo ninadhani serikali imebaini matumizi ya fedha hizo ni kinyume, ikaamua kuja na mfumo huo mpya ambao kwa kweli unaweza kunufaisha pande zote kuanzia wakopeshaji na wakopaji kwa ajili ya maendeleo.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Mama Salma Kikwete mwanamke wa shoka, amedhihirisha mkutano wanawake Afrika



Pascal Mayalla

**Jijini Bujumbura, Salma alishusha hoja 10 kwenye Mkutano wa Kimataifa wa Viongozi Wanawake wa Afrika uliofanyika hivi karibuni. Kwenye hoja zake 10, Mama Salma alianza na Rais Samia na kumaliza na Rais Samia. Kwanza, Salma Kikwete alianza kwa kuwasilisha salaam za kutoka kwa Rais Samia kwa mkutano huo na ukumbi ulimshangilia Rais Samia kama ishara kuwa wanawake wanaweza.**

KWA Maslahi ya Taifa leo, naomba niwapeleke jijini Bujumbura, Burundi ambako Mama Salma Kikwete, mke wa Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, alialikwa kuhudhuria na kuhutubia Mkutano wa Kimataifa wa Viongozi Wanawake wa Bara la Afrika ambao uliwakutanisha wake wa viongozi wakuu wa bara hili.

Nianze tu kwa kukumbusha, baada ya kushauriwa na kiongozi wetu mmoja kuwa tuhamie Burundi, baadhi yetu kwa hiari, baada ya ushauri huo, tumehamia Burundi, mimi nikiwemo, nimehamia Burundi na sasa naishi Bujumbura na kujitambulisha ubalozini na tulipokelewa vizuri. Nikiwa Bujumbura, nikajulishwa ujio wa kiongozi wetu, Mama Salma, nami nikaitika wito.

Baada ya mkutano na msaada wa Balozi wetu nchini Burundi, Dk. Jilly Maleko, nilipata fursa adimu ya kufanya mahojiano na Mama Salma, ndipo sasa nikagundua huyo mama kwanza ni mwanamke. Si mwanamke tu kama mwanamke wa kawaida, bali ni mwanamke wa shoka hasa. Ni mke kwa mumewe, Dk. Jakaya Kikwete, ni mama kwa familia yake, na pia ni mke wa Rais wa zamani (first lady) na ni Mkurugenzi wa taasisi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA). Kwa sasa ni mwanasiasa na mbunge wa Mchinga mkoani Lindi, akiwa mmoja wa wanawake wachache ambao ni majembe ya ukweli kwa kuwa mbunge wa jimbo.

Jijini Bujumbura, Salma alishusha hoja 10 kwenye Mkutano wa Kimataifa wa Viongozi Wanawake wa Afrika uliofanyika hivi karibuni.

Kwenye hoja zake 10, Mama Salma alianza na Rais Samia na kumaliza na Rais Samia. Kwanza, Salma Kikwete alianza kwa kuwasilisha salaam za kutoka kwa Rais Samia kwa mkutano huo na ukumbi ulimshangilia Rais Samia kama ishara kuwa wanawake wanaweza.

Pili, akauzungumzia umuhimu wa mkutano huo, huku akionyesha heshima ya mke mwema kuomba ruhusa kwa mumewe kabla ya kusafiri kwenda popote hata kwa safari za kikazi. Sijui ni wanawake viongozi wangapi bado wanawaheshimu hivyo wenza wao na kuomba ruhusa kusafiri hata kwa safari za kikazi.

Hoja ya tatu, aliwashauri wanawake wote hata walioolewa, wasiishie tu kuwa wake wema ndani ya familia zao, au wamama wema kwenye kulea familia, bali wajiongeze, wawe chachu ya maendeleo kwa kujishughulisha na shughuli nyingine zozote za kiuchumi kusaidia familia. Huu ni ujumbe mahususi kwa wanawake walioolewa wasiishie kuwa magolikipa.

Nne, Salma Kikwete ameitangaza vyema Tanzania na mambo mazuri yetu nje ya mipaka yetu, hivyo kuendelea kuifanya Tanzania kuwa nchi ya mfano barani Afrika. Kama mwanzo Tanzania ya Nyerere tulivyoitwa Kisiwa cha Amani kutokana na juhudi mbalimbali za Tanzania kuleta amani eneo la Maziwa Makuu, sasa Tanzania ya Samia inakwenda kuwa kitovu cha maendeleo ya biashara katika ukanda huu.

Jambo la tano, Salma ameinadi Tanzania kuwa nchi 'shamba darasa' la utetezi wa haki elimu kwa mtoto wa kike baada ya kuruhusu watoto wa kike wanaopata ujauzito wakiwa shuleni, kuruhusiwa kuendelea na masomo.

Hoja ya sita, Salma amewaasa viongozi wanawake, uongozi, madaraka na mamlaka, visiwafanye kusahau wajibu halisi wa mwanamke kwenye familia kuwa mke mwema na mama bora wa kulea familia. Kwa mantiki hiyo, mwanamke akiwa bosi, ubosi huo uishie kazini, akirudi nyumbani yeye ni mke na ni mama kwenye familia na mara moja moja, aingie jikoni.

Saba, Salma asisitiza ushirikiano baina ya wenza na kusisitiza umuhimu wa wenza kushirikishana kwenye kila jambo kwa waume kuwashirikisha wake zao kwenye mambo yao na wake kuwashirikisha waume zao kwenye mambo yao, kwa kujitolea mfano wa yeye na Jakaya.

Jambo la nane, Salma amesisitiza umuhimu wa kila familia kujipangia utaratibu wa maisha yao na kuishi kwa kuufuata utaratibu waliojipangia. Kwenye hoja hii amepiga ukungwi kidogo kuhusu maisha ya ndoa akisema: "akili ni nywele kila mtu ana zake" na "maisha ya ndoa, hayana shule."

Tisa, Salma asisitiza suala la maadili, kwa watoto na vijana, na kumpongeza Rais Samia anavyosisitiza maadili kwa viongozi na jambo la 10, amemalizia kwa hoja muhimu zaidi kuliko zote, hoja ya upendo kwa majirani akisisitiza mpende jirani yako kama ndugu yako.

Hakika ukiwa karibu na waridi lazima unukie uwaridi. Mtu kukaa katibu na Rais wa nchi kwa miaka 10, unakuwa na sifa za urais. Mtu kama huyu akiandaliwa kidogo tu, Tanzania tunaweza kujikuta tunampata Hilary Clinton wetu miaka ya karibuni.

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Hili la maji tusitende kazi kwa mazoea



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

KWA aliyesoma miaka ya nyuma, akiona wanafunzi wanasoma sasa hususan wa elimu ya sekondari mpaka vyuo vikuu, hakika atakuwa na sababu ya kuwahurumia kama si kuwasikitikia.

Zamani tukisoma, ukifika kidato cha nne na kukaribia kufanya mtihani wa mwisho kumalizia shule, tulikuwa tukipewa fomu za kujaza kazi (Sel Forms) kwa jinsi tulivyoona inafaa kwa mujibu wa chaguo.

Tulitakiwa kujaza nafasi tatu za kazi; unayoipenda sana, unayoipenda na nyingine ya ziada, kama hizo mbili za awali zitakuwa zimejaa. Kwa ufupi, ajira halikuwa tatizo, kazi ziliwatafuta watu.

Nafasi zilikuwa kedekede kwa sababu baadhi ya waliochagua walikuwa wakifaulu kuendelea na kidato cha tano, hivyo nafasi kutafuta kujazwa. Vivyo hivyo, tulipomaliza kidato cha sita, zililetwa fomu kama hizo kujaza ili kupata ajira.

Na wakati mwingine ulipochaguliwa ajira fulani ulikuwa na uwezo wa kukataa na kubadilisha. Hali iliendelea hivyo hivyo mpaka vyuo vikuu, hivyo kila aliyesoma alikuwa na uhakika wa ajira na ndiyo sababu wazazi walitilia mkazo watoto wao kusoma.

Leo hii, maliza kidato cha nne au sita au chuo kikuu hujazi fomu ila unarudi kwa baba na mama yako kutafuta cha kufanya, huku viongozi na wamotishaji wengine wakihanikiza watu kujiajiri baada ya kumaliza elimu zao kana kwamba kujiajiri kunakuja tu.

Wanaohanikiza vijana wamalizao elimu zao wajiajiri, wanahimiza vijana hao kuwa wabunifu na kutumia elimu zao kujiajiri na hata kuajiri wengine. Sikatai, inawezekana lakini ni kwa kiasi gani na idadi ipi ya vijana wenye ubunifu huo bila nyenzo.

Hatujasikia wafungwa wakimaliza vifungo vyao au wakitoka jela kwa msamaha wanashawishiwa kujiajiri. Zamani tukihubiriwa kuwa gerezani ni mahali pa mafunzo, kwamba mfungwa akitoka anakuwa tayari na ujuzi na kurudi mtaani akiwa mtu mwema na mwenye shughuli ya kufanya.

Lakini kama sasa hivi tunaambiwa Panyarodi wengi wao ni waliotoka magerezani, ina maana gani? Kama si kwamba huko huenda kufungiwa wasionane na ndugu zao na kufanyishwa kazi ngumu wakisubiri kumaliza muda wao na kurudi uraiani.

Haina tofauti leo na wanafunzi wanaokwenda shuleni na vyuoni kusubiri kumaliza miaka yao ya masomo na kurudi majumbani kama walivyotoka! Najiuliza, je wanaohanikiza vijana kutumia ubunifu kujiajiri wao wameutumia vipi kutuondolea kadhia hizi zinazotuzinga?

Leo hii inachekesha, kusikia nchi inapita kwenye mgawo wa maji! Inasikitisha kusikia, kwamba hata mikoa ya Kanda ya Ziwa inapitia kadhia hii wakati kuna Ziwa Victoria lenye maji ya kutosha.

Taifa lenye umri wa miaka 60 likiwa huru, leo bado linapiga kelele ya upungufu au ukosefu wa maji mpaka kuingiza wananchi kwenye mgawo. Miaka yote limekuwa na mawaziri wa maji lakini inashangaza mipango yao imekuwa ikiishia wapi na leo kutangaza mgawo wa maji!

Tunatangaziwa ukame ambao sasa umeanza kuua wanyama pori na punde utaingia kwa wanyama wafugwao kabla ya kuathiri na binadamu. Hivi sasa tunasikia wanyama wanavamia makazi ya watu kugombania maji! Ubunifu uko wapi katika hilo la maji?

Miaka yote tumekuwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa, tena ikifanya vizuri katika utabiri ikitarajiwa kuwa wanaotabiriwa hali hiyo watakuwa waangalifu na kuoanisha mipango yao na kuiweka sawa kwa ajili ya mustakabali mwema wa nchi.

Kinachoonekana ni kwamba wenye dhamana hutenda kwa mazoea na siku ikipita imepita na mwisho wa mwezi mambo swadakta, wanasubiri mwezi mwingine na miaka inakwenda, awamu zinaingia na kupita, lakini tatizo liko pale pale, maji.

Kutokana na hali inavyokwenda, kwa kuwa hatuna mipango madhubuti ya jinsi ya upatikanaji na matumizi ya maji, mpaka tunakuwa na mgawo mikoa yenye Ziwa kubwa kama Victoria, ina maana wizara husika zitagongana tu.

Namaanisha Wizara ya Maji lazima igongane na ya Mifugo na Uvuvi, lakini pia ya Maliasili kwani hizi zinahitaji maji ya kutosha wakati wote kwa ustawi wao. Ndiyo maana kuna haja ya kuunganisha wizara hizi na kuwa moja kwani zinahitaji rasilimali moja muhimu kabisa katika maisha maji.

Lakini wakati mchakato wa wazo hili ukifanyika, ni dhahiri wenye dhamana ya maji wakakaa chini na kubungua bongo na kuja na ubunifu, vinginevyo ikumbukwe mradi wa Bwawa la Umeme la Julius Nyerere unahitaji maji mengi sana. Kwa ukame huu tutafakari kabla ya hatari. Alamsiki!

# Shaka awatolea uvivu wabadhirifu serikalini

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, ametoa onyo na kuwatahadharisha watumishi wa serikali wanaojihusisha na ubadhirifu. Amesema watumishi hao wasijidanganye wala kuthubutu kujihusisha na vitendo hivyo kwa kuwa hawataonewa huruma.

Shaka alitoa kauli hiyo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa kongamano la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatumikia wananchi na kuwaletea maendeleo.

"Nataka kutahadharisha na kutoa rai kwa wote walioaminiwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuchunga dhamana zao lakini pia kuwa waadilifu hasa katika kusimamia fedha za miradi ya maendeleo. Ndugu zangu simba ni simba tu na simba hachezewi sharubu. Sasa niwaombe kila aliyepewa dhamana kuchunga maadili, lakini kila aliyepewa dhamana kuchunga dhamana yake.

"Wako watu wanadhani kwenye utawala huu wa Rais Samia Suluhu Hassan kutakuwa na mianya ya upigaji fedha za maendeleo.

Niwaambie watu hao wanacheza na moto. Rais Samia ni Mwenyekiti wa CCM hatakuwa na simile kwenye kuwavumilia wabadhirifu wa fedha za umma ambazo zimetolewa kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania.

"Nataka niwaambie hatavumiliwa mbadhirifu yeyote katika taifa hili. Pia hatavumiliwa yeyote mwenye dhamira ya kukwamisha ama kuhujumu miradi ya maendeleo ambayo inakwenda kuwanufaika Watanzania," alisema.

Shaka aliongeza kuwa kuna msemo mti wenye matunda ndio unaopigwa mawe, hivyo amewahakikishia kwamba Rais Samia yuko makini, imara na amejawa na utayari wa kuwatumikia Watanzania.

"Maneno maneno yasiwakatishe tamaa wala yasiwatoe imani kwa Rais wenu. Hakuna kurudi nyuma, Rais Samia amesimama imara na yuko madhubuti.

Tulikotoka ni kuzuri, tuliko ni pazuri zaidi na matarajio yetu tunakokwenda ni kuwa imara zaidi chini ya uongozi wa Rais Samia. Niendelee kuwasihi na kuwaomba tuendelee kumwombea Rais wetu, Mwenyezi Mungu ampe nguvu, uimara zaidi kuwatumikia Watanzania," alisema.

Kwa mujibu wa Shaka, uongozi wa Rais Samia umefungua matumaini mapya kwa Watanzania, furaha na mwanga wa maendeleo kwao na kwamba lengo kuu la Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025 ni kumkomboa mwananchi kutoka katika wimbi la umasikini.

Alisema katika kipindi chake cha mwaka mmoja na miezi minane, Rais ameimarisha diplomasia kwa mataifa jirani na ya nje katika sekta za kiuchumi na kisiasa.

"Rais Samia amezitembelea nchi takribani 22 na nchi yetu imeendelea kufunguka kiuchumi kupitia biashara na nchi za nje. Takwimu za hivi karibuni zimerekodi ongezeko kubwa la mauzo ya nje kwa bidhaa na huduma za Tanzania katika nchi mbalimbali za Afrika Mashariki," alisema.

Aliongeza kuwa, takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Takwimu ya Kenya, zimeonyesha kukua maradufu kwa mauzo ya Tanzania katika nchi hiyo kwa takribani Sh. bilioni 20.5 kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2021/22 kutoka Sh. bilioni 10.8 kwa mwaka uliopita wa 2020/21.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Mughanga, Manispaa ya Singida, Pascal Kichambati (wa pili kushoto), wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule hiyo, jana. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# RC awaweka njiapanda Ma-DED ujenzi madarasa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameagiza wakurugenzi wa halmashauri zote mkoani hapa kusimamia ujenzi wa vyumba 290 vya madarasa na kuhakikisha unakamilika kabla ya Desemba 15, mwaka huu.

Amesema kukamilisha kwa ujenzi huo mapema, kutawezesha wanafunzi watakaochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwakani kuanza masomo bila usumbufu wowote.

Serukamba alitoa agizo hilo jana baada ya kufanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika halmashauri za Manispaa ya Singida na za wilaya ya Ikungi na Manyoni.

"Kama tulivyokubaliana ujenzi wa madarasa yote 290 ambayo serikali imetoa Sh. bilioni 5.8 katika mkoa wetu uwe umekamilika kabla ya Desemba 15, mwaka huu," alisema.

Akikagua ujenzi wa vyumba vya madarasa sita katika Shule ya Sekondari ya Mughanga, Manispaa ya Singida, alimwagiza Mkurugenzi wa Manispaa, Jeshi Mzalendo, kuunda kamati ambayo itakuwa inapita kila siku jioni kuangalia maendeleo ya ujenzi huo.

Pia alielekeza fedha zitakazokuwa zimebaki wakati wa ujenzi huo utakapokuwa umekamilika, zitumike kwa ajili ya kununua madawati.

Mzalendo alimhakikishia mkuu wa mkoa kuwa ujenzi wa vyumba 50 vya madarasa ambayo manispaa imepewa na serikali Sh. bilioni moja, utakamilika Novemba 30, mwaka huu.

Mzalendo alisema ujenzi wa vyumba vya madarasa katika manispaa hiyo uko katika hali nzuri, isipokuwa katika shule za sekondari za Unyanga na Mfumu ambako mchakato wa kuzihamisha fedha ulichelewa lakini suala hilo limeshapatiwa ufumbuzi na kazi imeshaanza.

Akiwa katika wilaya ya Ikungi alitembelea ujenzi wa madarasa katika shule za sekondari za Ikungi na Unyahati.

Mkurugenzi Mtendaji wa wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi, alisema serikali imetoa Sh. milioni 580 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 29 katika halmashauri hiyo.

Alisema ujenzi wa madarasa 20 uko katika hatua nzuri na kwamba kabla ya Desemba 15, yote yatakuwa yamekamilika.

## Neema yaja Watanzania mafuta na gesi

**Na Mwandishi Wetu**

MAJADILIANO kati ya serikali na wawekezaji ya kuanza uchakataji wa gesi asilia iliyosindikwa ( LNG) yako katika hatua za mwisho na kwamba mradi huo unatarajiwa kuanza wakati wowote.

Kutokana na mchakato huo, Watanzania wametakiwa kujiandaa kunufaika na shughuli za mafuta na gesi asilia nchini.

Kamishna wa Mafuta na Gesi Asilia wa Wizara ya Nishati, Michael Mjinja, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam, wakati wa mkutano wa wadau wa mafuta na gesi uliohusu utambulisho wa mfumo mpya wa kusajili wadau wote katika sekta hiyo.

Mkutano huo ulioandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), uliwakutanisha wadau katika mnyororo wa mafuta na gesi wa ndani na nje ya nchi ili kubadilishana mawazo na uzoefu.

Mjinja alisema ushiriki wa Watanzania kwenye shughuli za mafuta na gesi asilia zimepewa kipaumbele katika sera, sheria na kanuni zinazosimamiwa na Wizara ya Nishati.

Alisema Wizara ya Nishati kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na PURA, imeendelea kuhakikisha kampuni zinazoshiriki kwenye utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi, zinatoa fursa kwa Watanzania katika ajira na huduma mbalimbali.

Kamishna huyo alisisitiza kwamba ni vizuri Watanzania wakajiandaa kunufaika na fursa zitakazojitokeza kwenye mradi huo, huku akitolea mfano mradi wa LNG ambao uko kwenye hatua ya majadiliano na wawekezaji kwamba utakuwa na fursa nyingi.

Ili kuogeza ushiriki wa wazawa, Mjinja alisema serikali imechukua hatua kadhaa zikiwamo kuanzisha mitaala ya mafuta na gesi kwenye baadhi ya vyuo vikuu, kusomesha watumishi na kuanzisha idara na vitengo vya ushiriki wa wazawa.

Mkuu wa Kitengo cha Ushirikishwaji wa Wazawa na Uhusishwaji wa Wadau, Charles Nyangi, alisema PURA imeanzisha mfumo wa usajili wa watoa huduma katika mafuta na gesi ili kuwatambua wote wanaohusika.


"Umuhimu wa mfumo huu ni kuwa na taarifa za wangapi wamesomea mafuta na gesi, wangapi wameajiriwa kwenye sekta hii, wangapi hawajaajiriwa na wangapi wananufaika na mnyororo wa thamani,"

# MAISHA Jumapili

NOVEMBA 6, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Ukurasa 15

## Huisha nyumba yako uifurahie



Ukurasa 14

## SHATI LA DRAFTI Mwonekano wa urembo, utanashati



12 MAISHA JUMAPILI NOVEMBA 6, 2022



Paskazia Casmir

'Bridal shower' ya **Paskazia Casmir** iliyofanyika Oktoba 29 Cozy cafe Kinondoni, anayetarajiwa kufunga ndoa na **James Semiono**, Send-off yake imefanyika jana katika Ukumbi wa Primrose-mbezi beach. Na baada ya hapo, harusi itafuata. Hii itakuwa Novemba 12 katika Parokia ya Mtakatifu Francis De Sales-Mkuza, Kibaha mjini.


Ukurasa 12




# NG'ARISHA USO Vitu hivi huondoa chunusi

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | D | U | N | D | A |
| ■ | U | ■ | ■ | E | ■ |
| U | M | A | ■ | R | ■ |
| ■ | A | ■ | B | E | I |
| ■ | Z | ■ | ■ | V | ■ |
| W | A | N | G | A | ■ |

## AMSHA AKILI





## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI







MTOTO Musa alikuwa akizungumza na mama yake, katika maongezi yao alianza kumuuliza kuhusu asali.

Musa: Eti mama, kila mlamba asali huwa anarudia?

Mama: Ndio mwanangu, hiyo ni kutokana na utamu wa asali.

Musa: Kwa hiyo kila anayelamba asali lazima achonge mzinga?

Mama: Hapana mwanangu, mzinga wanachonga wafugaji na sio walaji.


Musa: Mbona mwalimu katuambia ukionja asali lazima urudie?

Mama:Huo ni msemo tu, ukimaanisha kila mtu anayefanya jambo kwa ubaya lazima atarudia kama hataonywa.

SWALI

Ziwa Rukwa linapatikana mkoa gani?

## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
IGA, UMA, JANGA, JEMBE, JAMBIA, BONGEA

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Madhara wanaodharau wazazi yako mbele yao

KARIBU msomaji wangu tutafakari jinsi Maisha Yalivyo. Wiki kadhaa mfululizo tuliona kisa cha binti daktari aliyemdharau mama yake akafa kwa uchungu, huku yeye akiishia kuishi na kula jalalani. Hebu tujiulize wapendwa, hivi kuna ubaya gani kumheshimu mzazi wako? Kulikuwa na ubaya gani kwa yule binti daktari kumtii na kumheshimu mama yake mzazi aliyemlea kwa mahangaiko makubwa?

Hata pale mama alipomtafuta amwone kwa macho, kulikuwa na ubaya gani kumkaribisha ili ampe taarifa namna alivyofanikiwa hadi pale alipo. Ilikuwa wakati wa kufurahia pamoja. Lakini muda wote miaka 14 binti alikuwa akifurahia na marafiki zake na kumsahau mama yake!

Alijikuta anaishia kula na kuishi majalalani kwa sababu ya kumdharau mama yake. Mama ambaye alijitoa maisha yake, alijikataa maisha yake akayapa maisha ya mwanae kipaumbele.

Wazazi wengi wako hivyo. Wanahatarisha hata maisha yao kwa ajili ya watoto wao. Lakini watoto wanapopata nafasi wanawashusha moyo wazazi. Wanawakatisha tamaa kwa sababu ya kufanikiwa na kuwasahau.

Kijana unamwona mzazi wako kama si kitu. Daktari alifanikiwa na kumwona mama yake si kitu wakati alikuwa chanzo cha mafanikio yake hayo.

Lakini laiti angefunguliwa macho ya kiroho akakumbuka jinsi mama yake alivyokuwa akishona nguo zake za shule kwa mkono wake. Jinsi alivyokuwa anamwogesha, kumsugua miguu, kumvisha nguo nzuri na kumhimiza awahi shuleni.

Naye mama anawahi kibaruani ili binti akirudi kutoka shuleni akute chakula. Yote haya binti aliyasahau. Leo anamwambia mamaye usiniguse, usinisogelee. Hakuna atakayejisikia vizuri kwa kauli hizo.

Hata ukiwa na nafasi kubwa namna gani, katu usiwadharau wazazi wako. Usifanye kama huyo daktari aliyeungana na marafiki, akamdharau mama yake. Mama alitoa utu wake kwa ajili yake.

Mama alikataa wanaume kwa ajili yake, kwamba niko tayari nife masikini lakini mtoto wangu atimize ndoto zake. Lakini mtoto huyu hakujali hisia za mama yake, akamvunja moyo. Mama huyu alikufa katika mazingira magumu na kuzikwa na mtu asiyemfahamu!

Angalia katika maisha yako ni kwenye vipengele vipi umemdharau mzazi wako. Kisa hiki msomaji wangu natamani kijenge wengi kwa jinsi wanavyoenenda kimaisha. Jiangalie na wewe usije kesho kuwa mfano.

Yako matukio mbalimbali yanayowapata watu katika maisha. Jiulize kisa hiki cha daktari kama ingekuwa ni wewe ungefanya nini. Kila mzazi anapenda kuheshimiwa na watoto wake.

Heshima ni amri ambayo Mungu aliiweka kwa wanadamu, yenye ahadi, pale aliposema: 'Waheshimu baba yako na mama yako, amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi, upate heri, ukae siku nyingi katika dunia". Hapa tunaonywa tusipoheshimu wazazi hatutaishi siku nyingi hapa duniani!

Ni muhimu sana kutengeneza mahusiano yako na mzazi wako. Haijalishi mzazi/wazazi wana kiwango cha chini cha elimu. Wapo wazazi wengi hawakusomeshwa na wazazi wao, lakini watoto wao walihakikisha wanasoma vizuri, kama alivyofanya mama wa binti daktari.

Ukifanikiwa, rudi wasaidie wazazi wako. Mungu ameweka misingi mizuri sana kuhusu malezi na uhusiano katika maisha yetu. Lakini maarifa hayo wengi hawayatafuti. Wanatumia akili zao wenyewe.

Mungu anasema kwenye andiko lake kwamba, ''Mtumainie Mungu kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe (Mithali 3:5). Pia anasema: "Na alaaniwe amdharauye baba yake au mama yake. Na watu wote waseme, Amina.

Vijana wengi kizazi cha leo wanadharau sana wazazi wao. Hata pale wanapoonywa kuacha tabia fulani wamekuwa wakiwapuuza, matokeo yake yanawapata majanga wanashindwa kujinasua.

Wanaonywa kwamba usitumie dawa za kulevya, wanapuuza, acha kushikamana na kikundi fulani cha wahuni au majambazi, wanapuuzia. Matokeo yake vijana wa aina hii wamejikuta matatani na wengine hata kupoteza maisha katika mazingira ya kutatanisha licha ya kwamba awali walishaonywa lakini hawakujali, wakapuuzia.

Kumbe unapodharau na kutotii wazazi, iko adhabu mbele yako. Maagizo ya Mungu yako wazi pale anaposema: "Jicho la mtu amdhihakiye babaye, na kudharau kumtii mamaye; kunguru wa bondeni wataling'oa, na vifaranga vya tai watalila." (Mithali 30:17).

***Msomaji wangu, yatupasa wote kwa rika zote kuwaheshimu wazazi wetu. Hata kama umefanikiwa kwa kiwango gani, usithubutu kumdharau mzazi wako. Maisha Ndivyo Yalivyo! Hadi wiki ijayo. Una kisa? Ujumbe 0715268581***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# COP27 imeanza Misri, Watanzania tufuatilie inatuhusu

MOJA ya matatizo makubwa yanayoikabili dunia, Tanzania ikiwamo, ni kasi ya mabadiliko ya tabianchi ambayo yamesababisha madhara mengi kama sasa tunavyoshuhudia hakuna mvua za kutosha. Ukame uko kila mahali huku binadamu na wanyama wakipoteza maisha kwa kukosa maji na malisho.

Mabadiliko ya tabianchi hayasababishwi na eneo fulani pekee bali mchango wa dunia kwa ujumla, huku nchi za Afrika kwa ujumla wake zikichangia hewa ukaa chini ya asilimia nne na nchi zilizoendelea zikichangia kwa kiasi kikubwa.

Kwa Tanzania, mathalan, mtu mmoja anachangia gesi ukaa kwa asilimia 0.22 kwa mwaka huku China na Marekani zikichangia asilimia 26 kwa kipindi hicho hicho. Hii ni kutokana na shughuli za viwanda na nyinginezo ndiyo maana nchi hizo zinatoa fedha za kusaidia kukabili kwa nchi zilizotunza mazingira.

Hadi sasa hakuna mpango kwa nchi hizo kupunguza viwanda na ndiyo kwanza vinaongezeka na ziko tayari kuendelea kutoa fedha kwa nchi zinazochangia kupunguza hewa ukaa kwa kutunza mazingira.

Kwa sasa kila eneo linakabiliwa na ukame huku maji ambayo ni muhimu kwa kila kiumbe yakiendelea kupungua, migogoro baina ya binadamu na binadamu; wanyama na binadamu inaongezeka kwa sababu raslimali hiyo inapotea katika maeneo mengi. Ukisafiri kwa anga utaona hali ilivyo ardhini, lakini kasi ya kupaa kwa bei ya nafaka kulikochagizwa na kupaa kwa bei ya mafuta ni udhihirisho kwamba ukame ni tishio. Pia unaona mito na maeneo mengine yalivyokauka.

Hivi karibuni, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilieleza kuwa mikoa 14 inayopataga mvua za vuli hazitakuwepo na kwamba ukame utaendelea kutamalaki.

Mkutano wa mabadiliko ya tabia nchi COP27 ulioanza leo jijini Cairo, Misri, unawaleta pamoja wakuu wa nchi 100 na washiriki wengine 35,000 ikiwa ni mwaka mmoja tangu COP26 ifanyike Scotland ilioweleta pamoja wakuu wa nchi 120 na washiriki wengine 40,000.

Katika mkutano huu, Afrika itawasilisha mambo sita ambayo ni kutotimizwa kwa ahadi ya kutoa Dola bilioni 100 kila mwaka hadi mwaka 2020 kwa nchi zilizoathiriwa na mabadiliko ya tabinchi ikiwa ni ahadi ya nchi zilizoendelea tangu mwaka 2009 ambazo zinazalisha hewa ukaa kwa wingi.

Pia zitatoa fidia ya uharibifu uliosababishwa na mabadiliko ya tabia nchi, kwamba Afrika imechangia uharibifu kwa asilimia 0.04 lakini ndiyo inayobeba mzigo mzito licha ya kwamba jambo hilo halijapewa kipaumbele na sasa litasukumwa zaidi kwenye mkutano huu.

Ahadi nyingine ni kupunguza hewa ukaa kwa nyuzi joto 1.5 hadi mwaka 2030, lengo ambalo halionyeshi dalili hasa kwa nchi zilizoendelea ambazo zina viwanda vingi vinavyozalisha hewa ukaa.

Lingine ni kuhama kutoka matumizi ya nishati chafu kwenda kwenye nishati safi, kuacha kutumia makaa ya mawe na kuhamia kwenye gesi,jua na joto ardhi.

Hadi sasa tunaona uhaba wa nafaka huku ikizidi kupanda bei, ongezeko la migogoro baina ya binadamu na wanyamapori ambao wanatoka maeneo yaliyohifadhiwa kwenda kutafuta malisho, huku binadamu nao wakivamia maeneo ya hifadhi kupata mahitaji ya Wanyama wafugwao.

Kwa sasa maji ya bahari na maziwa yanaingia kwenye makazi ya watu kutokana na kuongezeka kwa kina cha maeneo hayo. Maeneo yaliyokuwa yanafaa kwa kilimo hayafai tena kwa sababu maji ya chumvi yameharibu ardhi, pia majisafi hayapatikani tena. Aidha, mito na maziwa yanakauka huku mabwawa yakikosa maji kabisa. Hivi karibuni, kwa mfano, wananchi wa Monduli waliiomba serikali kuwapelekea maji kwa kuwa hali ni mbaya sana.

Jitihada nyingi zimefanyika ikiwamo kuhamasisha wananchi kutunza mazingira, kupanda miti kwa wingi na kuachana na matumizi ya nishati ya kuni, ingawa bado kuna kazi kubwa ya kufanya kwa kuwa mkaa unatumika zaidi kutokana na kupaa kwa bei ya gesi.

Hali ya upatikanaji wa chakula ni ngumu sana kwa sasa, nafaka zimepanda bei hali ya maisha inakuwa ngumu kutokana na visababishi vingine kama kupanda kwa bei ya mafuta kutokana na vita ya Ukraine na Russia pamoja na UVIKO -19.

Mabadiliko ya tabianchi si jambo la kulichukulia kirahisi, hivyo ni lazima nchi iendeleze mikakati yake ya kusaidia wananchi wake kuishi na hali hiyo ambayo haiwezi kuisha leo wala kesho kutokana na kasi ya ukuaji wa maendeleo.

Lazima jamii yetu iendelee kuelimishwa namna ya kutumia fursa katikati ya matatizo, mathalani kwa sasa kuna biashara ya hewa ukaa kwa wananchi waliotunza misitu ya asili, misitu ya kupanda na binafsi ambayo wanauza duniani kwa nchi zinazoharibu mazingira.

Misitu hiyo inasaidia kupunguza hewa ukaa kwenye anga na kukabili hali iliyopo sasa ya vipindi vya mvua kutoeleweka, ukame wa muda mrefu, joto na baridi kali kiasi cha kuathiri binadamu na viumbe wengine kama tunavyoona sasa maeneo mengi yana joto kali hadi misitu inawaka yenyewe na kwingine baridi sana. Usalama wa chakula kwa sasa uko hatarini kwa kiasi kikubwa. Wananchi hawana uhakika wa mlo kamili kutokana na kutokuwa na uhakika wa chakula chenyewe ili waendelee kuwa hai.

Kwa mantiki hiyo, kupambana na mabadiliko ya tabianchi ni lazima kwa kila mmoja lakini wananchi kutumia mbinu zao na za jumla kukabili hali hii ili dunia iwe salama kwa kila mmoja anayestahili kuifurahia.

Tunasikia migogoro baina ya wanyama na binadamu inashamiri, wanyama wanatoka kwenye maeneo yao ya asili kutafuta malisho na binadamu anapeleka mifugo maeneo yaliyohifadhiwa kutafuta malisho. Hii inafanya maisha yasiwe na amani kwenye maeneo mengi.

Mabadiliko ya tabianchi ni tishio lazima tuwe na mbinu zinazotekelezeka, kubuni namna ya kuendelea kupata maji ya mahitaji ya nyumbani na kilimo cha umwagiliaji kwasababu cha mvua hakijaonyesha manufaa chanya.




# Paskazia Casmir

'Bridal shower' ya **Paskazia Casmir** iliyofanyika Oktoba 29 Cozy cafe Kinondoni, anayetarajiwa kufunga ndoa na **James Semiono**, Send-off yake imefanyika jana katika Ukumbi wa Primrose-mbezi beach. Na baada ya hapo, harusi itafuata. Hii itakuwa Novemba 12 katika Parokia ya Mtakatifu Francis De Sales-Mkuza, Kibaha mjini.

## MITINDO



# SHATI LA DRAFTI

## Mwonekano wa urembo, utanashati

MASHATI ya Drafti yamepata umaarufu kutokana na rangi, na michoro yake kuwa na mwonekano unaovutia.

Nguo za aina hii zinaweza kuvaliwa sehemu yoyote, lakini inapendeza zaidi kuvaliwa katika matembezi, sherehe na sehemu za mapumziko.

Kimsingi mashati ya drafti hayachagui aina ya nguo zinazoambatana nazo, kwa mfano unaweza kuvalia na suruali ya kawaida na inapendeza zaidi na jinzi.

Mchanganyiko wa michoro ya pembe nne ya rangi nyeusi na nyeupe, bluu na nyekundu au nyekundu na nyeupe ni aina ya mashati yanayopendwa zaidi na vijana.

Katika mpangilio huo, mvaaji hana sababu ya kueleza hajapendeza kwani macho ya watu wanaomwangalia yanaweza kutoa majibu sahihi, kuwa yuko bomba.

Kama unatoka katika matembezi ya jioni, pigilia shati lako la drafti, suruali ya jinzi, chini kumbuka kuvaa raba au kwa wanawake wenye mapenzi na viatu virefu wanaweza kuvitumia. Kama unataka kuweka nakshi zaidi tundika jaketi pamoja na kofia kichwani.



UREMBO

Na Mary Geofrey

# NG'ARISHA USO
## Vitu hivi huondoa chunusi



WAKATI watu wengi wakitumia mafuta pia na losheni zenye viambata vyenye sumu huharibu ngozi zao za uso kwa nia ya kuondoa chunusi.

Hata hivyo kuna njia za asili za kuaminika za kuondoa chunusi na hazihitaji pesa nyingi kutumia.

**Kipande cha barafu**

Barafu husaidia kukausha/kunyausha chunusi na kunyonya mafuta na kuyasambaza katika maeneo mengine ya mwili.

Chukua barafu tia kwenye kitambaa safi halafu fanya kama unasugua taratibu sehemu yenye chunusi.

Fanya hivyo mara nyingi uwezavyo.

**Dawa ya Meno**

Dawa ya maajabu ya kuondoa chunusi haraka bila kuacha kovu, inakausha chunusi haraka sana.

Chukua dawa kidogo weka eneo lenye chunusi mpaka asubuhi halafu nawa uso kwa maji safi

**Kitunguu Saumu**

Kitunguu hutibu magonjwa takribani 20 pia chunusi kwa uharaka sana.

Kata kitunguu swaumu vipande viwili, kisha sugua taratibu eneo lenye chunusi.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# KATA KAROTI, HOHO

JIKO linahitaji ujuzi wa mambo katika kuandaa vyakula ili kupata ladha utakayoifurahia.

Leo tuelekezane namna mbalimbali za kukata viungo jikoni na kwanini ufanye hivyo.

Tutajifunza namna ya kukata karoti na hoho ili kujua kuna umuhimu gani au kwanini ukate hivi na sio vile.

**Karoti za duara**

Uandaaji wa karoti kwa umbo hili unategemeana sana na matumizi. Ninaposema matumizi namaanisha unaitumia kwenye chakula gani au kwenye mboga gani.

Mara nyingi kama utaandaa karoti zako kwa namna hii basi ni vyema ikawa kwa ajili ya matumizi ya mapishi kama ya wali , pilau, supu na dagaa.

Mbali na muonekano mzuri katika chakula ukataji huu huweka wepesi wa kuiva na karoti kubaki katika umbo lake.

Karoti za urefu

Kuandaa karoti kwa urefu kuna aina mbalimbali ikiwamo nyembamba na nene pia.



Ukubwa au upana wa karoti yako unayoiandaa kwa urefu unategemeana na unahitaji kuitumia kwenye chakula gani.

Karoti nyembamba mara nyingi inatumika kwenye kachumbari kutokana na kwamba haimpi shida mtumiaji na ni rahisi kutafunika.

Zenye upana zaidi hutumika kwenye makange, mboga nyingi pia waweza kutumia karoti zenye umbo hili.

Karoti ya kusaga

Namna hii ya uandaaji wa karoti ndio namna inayotambulika kwa wengi na wengi hutumia kwenye kila pishi.

Hii ni kwasababu ni nyepesi sana lakini pia ni rahisi sana kuiva na kuacha ladha yake kwenye pishi lako.

Njia hii ni nzuri kwa ambao hawapendi kutafuna karoti wakati wa kula kwani kiungo hicho huiva na kupotelea kwenye mchuzi.

Maandalizi ya hoho

Katika uandaaji wa hoho nako kuna aina mbalimbali za kuziandaa.

Uzuri wa kila aina ya uandaaji wa hoho hauna kikomo cha matumizi isipokuwa tu zile zinakatwa kwa ajili ya makange, ambazo hukatwa kwa urefu lakini tofauti na hapo unaweza kukata au kuandaa hoho kwa namna yoyote unayoipenda na ukatumia katika chakula chochote.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Huisha nyumba yako uifurahie

NYUMBA ni kitu muhimu kwa mwanadamu katika maisha yake ya kila siku. Nyumba ni sehemu ambayo humpa mtu malazi na amani iwapo itakuwa na mazingira mazuri.

Kwa ujumla, nyumba au malazi ni moja ya mahitaji muhimu matatu mengine yakiwa mavazi na chakula. Kutokana na ukweli huo, wengi wetu tunapenda ndani ya nyumba zetu kuwe kuna mvuto wa kuridhisha nafsi zetu.

Kwa maneno mengine, ubora na unadhifu wa nyumba humfanya mtu kufurahia mazingira na hata kuwa na amani ya moyo na kupenda mara kwa mara awapo nyumbani. Kinyume cha hapo, mtu huyo ataichukia nyumba na kutumia muda mfupi wa kukaa hapo.

Pamoja na kupenda huko, tumekuwa tukishindwa kuziridhisha nafsi, sababu kubwa ikiwa kukosa kipato cha kutuwezesha kutengeneza nyumba zetu kama nafsi inavyopenda.

Wataalam wa masuala ya ujenzi, Lucas Kwambikwa, anasema ziko njia mbalimbali za kufikia angalau kwa kiwango fulani ambacho kinaweza kuridhisha nafsi kwa kuboresha nyumba yako ikawa na mvuto bila kutumia gharama kubwa.

Lucas anasema endapo nyumba yako imechakaa na haufurahishwi na mwonekano wake, unaweza kufumua rangi yake na kupaka upya na inaweza kuwa ile ile au ukabadilisha nyingine ili mradi uwe umeridhika nayo ili kuipa muonekano mpya.

Pia anasema kubadilisha samani za ndani nayo inachangia kupa mwonekano mpya nyumba yako kwamba hata kama huna ya kuweka mpya, unaweza kuzifanyia ukarabati mdogo ikiwamo kubadili kitambaa kama ni za kukalia sebuleni.

Mbali na samani, mapambo nayo yatakupa mwonekano mpya, kama uliweka na yana muda mrefu yamechakaa weka mengine mapya.

Anasema ni muhimu kuwa na picha yako kichwani ya namna unavyotamani kubadili nyumba yako ili kila unachofanyia marekebisho kiendane na matakwa yako.

Lucas anashauri kuondoa ndani ya nyumba vitu ambayo havitumiki ili kuacha nyumba kuwa na hewa ya kutosha na kukupa kufurahia kukaa muda mwingi bila kuchoka.

"Kwa mfano badala ya kuweka vitu vingi ukutani, ukatafuta picha moja kubwa ya mvuto na kuibandika, hiyo haitamchosha mtu kutazama," anasema.

Anashauri kuepuka kununua vitu vingi na kuviweka ndani ya nyumba kabla ya kufahamu matumizi yake na kwamba ni vema kuhakikisha kwamba kila kitu kinachowekwa ndani ni kile kinachotumika.

Anataja baadhi ya vitu vya msingi vya kuzingatia unapohuisha mwonekano wa nyumba yako kuwa ni pamoja na pazia au zuria kwamba wakati wa kuviweka ni muhimu kuhakikisha rangi zake ni zile zinazoshabihiana na vitu vilivyo ndani ya nyumba.

"Nyumba ni ubunifu, ukizingatia hili utafurahia nyumba yako na utapenda kukaa humo bila kuchoka," anasisitiza.



## Namna ya kuandaa meza ya chai




JE ndani ya nyumba kuna utaratibu wa kuandaa meza ya chai nyakati za jioni na asubuhi? Basi kama huna unaweza kusoma makala hii kufahamu jinsi gani unaweza kuandaa meza yako ya chai.

Hivi ni baadhi ya vitu vinavyotakiwa kuwekwa juu ya meza ya chai kabla ya watu kujumuika kufurahia ladha tamu ya chai.

1. Meza inapaswa kufunikwa na kitambaa kizuri kwa ajili ya kuwavutia walaji.
2. Kila kiti cha mtu, weka sahani, leso juu yake, pia kulia kwa sahani kuna kisu, weka kushoto uma.
3. Katikati ya meza ya chai weka biskuti na chombo cha jam, maziwa na sahani ya limau.
4. Vyombo vya chai ni lazima kuwepo na vikombe, chupa na chombo cha sukari.
5. Ikumbukwe kwamba wanawake hupewa kikombe cha chai na kisosi, na kwa wanaume glasi ya chai kwenye kishikizi.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
NINI TENA?
'FEDHWA ZA MIRADI'
UNAMTONGODHA NANI? MAPENZI YAKO YAULAGHAI ILI UNIPUKUTISHE SITAKI... NSHASEMA!
KAPUKU
BAR
HAWA BHANA 'VINJUNGA' VYAO VITANIPOFUA MACHO!
BONGO FLEVA
NDUGU HUKU WAPI MBONA UNATAKA KUNITIA JAKAMOYO MWENZAKO!
WEWE SI UMEJINADI NI MTATA UTALIPIA HUKU NAULI YAKO
GHETO LA MASELA
WAPANGAJI KAMA WAKOROFI TIMUA WOTE ROHO IKUPOE
WAKIJA KUPANGA WALIOPOA NYUMBA ITADOROLA HAKUNA HEKAHEKA!
ANGALAU TOKA NIPIGE MARUFUKU MAKTABA IMEKAUKA
KADI ZILIJAA KAMA FEDHA BENKI KUU
KADI
MIALIKO
USWAZ
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UKIWAZA NA KUWAZUA HUKOSI KUAMBUA...

# Zelensky ajigamba sasa wapo Donbass

**KYIV,** UKRAINE

RAIS Volodymyr Zelensky wa Ukraine amesema mapigano makali yanaendelea na sasa yamejikita katika eneo la Donbass karibu na miji ya Bakhmut na Soledar katika mkoa wa Donetsk.

Kauli hiyo inakuja katika kipindi ambacho Russia ikiwa katika mpango wake wa kuongeza wanajeshi wa akiba zaidi ya 300,000 kwa ajili ya kufanikisha uvamizi katika maeneo hayo.

Zelensky alisema wapo katika udhibiti, huku Russia tayari imepoteza maelfu ya wanajeshi wake katika eneo hilo. Kwa mara nyingine Zelensky amesisitiza kwamba Ukraine itapigana hadi ifanikishe kuirejesha kwa ukamilifu mipaka yake ya asili.

Wakati huo huo, wafungwa wa mauaji waliopatikana na hatia na wauzaji dawa za kulevya ambao wametoka gerezani hivi majuzi nchini Russia wanaandikishwa kupigana vita nchini Ukraine chini ya mabadiliko ya sheria.

Rais Vladimir Putin aliifanyia marekebisho sheria ya kuwaita askari wa akiba na kuwajumuisha wanaume waliopatikana na hatia ya uhalifu mkubwa ambao walitoka gerezani hivi majuzi.

Wafungwa wa zamani waliopatikana na hatia ya uhalifu wa ngono dhidi ya watoto au ugaidi bado hawajajumuishwa katika mpango huo.

Wanajeshi wa Russia wameshutumiwa kwa uhalifu wakati wa uvamizi wa Ukraine.

Tume Huru ya Kimataifa ya Uchunguzi kuhusu Ukraine, iliyoundwa na Umoja wa Mataifa mwezi Septemba iliripoti kwamba uhalifu wa kivita ulifanywa na vikosi vya Russia ikiwa ni pamoja na mauaji ya raia na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia.

Russia inakanusha kushambulia raia kimakusudi na inashutumu vikosi vya Ukraine kwa kushambulia maeneo yanayoshikiliwa na watu wanaotaka kujitenga nchini humo, jambo ambalo Ukraine inakanusha.

Tume ya Umoja wa Mataifa ilisema imegundua matukio mawili yaliyotendwa na wanajeshi wa Russia na Ukraine lakini idadi ya tuhuma za uhalifu wa kivita dhidi ya Russia ilikuwa kubwa.

**BBC**



Waandishi wa habari wakilia na kuomba msaada karibu na mwili wa mwenzao aliyepigwa na bomu la machozi walipokuwa wamekusanyika katika kituo cha polisi cha Delmas 33, wakitaka kuachiliwa kwa Robest Dimanche aliyekuwa kizuizini wakati akifuatilia maandamano katika mji wa Port-au-Prince, nchini Haiti. **PICHA: AFP**

# Korea Kaskazini yazidi kufyatua makombora

**PYONGYANG,** KOREA KASKAZINI

KOREA Kaskazini jana imefyatua makombora manne ya masafa mafupi kuelekea baharini.

Taarifa hiyo ambayo imetolewa na jeshi la Korea Kusini inaonyesha hatua hiyo ni ya hivi karibuni ya ufyatuaji makombora.

Ilifafanua kuwa jeshi limegundua hatua hiyo iliyotekelezwa kutokea jimbo la Pyongan, la Korea Kaskazini, upande wa magharibi ya bahari.

Ufyatuaji huo umefanyika katika majira ya saa tano na dakika 32 hadi 59. Muendelezo wa hatua hiyo ya Korea Kaskazini unajumuisha ufyatuaji wa kombora la masafa marefu na moja kati ya hayo lilitua katika eneo la bahari la Korea Kusini, ikiwa ni mara ya kwanza tangu kumalizika kwa Vita vya Korea 1953.

Jaribio hili la sasa linafanyika katika kipindi ambacho Marekani na Korea Kusini zikifanya mazoezi yao makubwa zaidi kuwahi kutokea katika jeshi la anga, ambayo Korea Kaskazini iliyokasirishwa iliyaeleza kuwa ya kiuchokozi.

**DW**

# Mgomo wa marubani waendelea Kenya

**NAIROBI,** KENYA

WAZIRI wa Usafirishaji wa Kenya Kipchumba Murkomen, amesema safari za ndege za shirika la ndege la Kenya, Kenya Airways zimevurugika kutokana na mgomo wa marubani wake ambao wanashinikiza uwepo wa mazingira mazuri ya kazi.

Hatua hiyo imesababisha ndege kadhaa kushindwa kufanya safari zake, hali ambayo imewaathiri maelfu ya abiria.

Waziri huyo mpya wa Usafrishaji Murkomen, aliwaambia waandishi wa habari katika uwanja wa ndege jana kwamba mgomo huo haukuwa na msingi ni sawa na uhujumu uchumi.

Shirika la ndege la Kenya, ambalo linamilikiwa kwa sehemu fulani na serikali ya Kenya pamoja na lile la Ufaransa, Air France na la Uholanzi, KLM, ni mojawapo ya mashirika makubwa zaidi ya usafiri wa anga barani Afrika, linaloziunganisha nchi nyingi za Ulaya na Asia.

Hata hivyo, linakabiliwa na misukosuko, ikiwa ni pamoja na kupata hasara kwa miaka kadhaa.

**DW**

# Waokolewa baada ya kuwa chini ya mgodi siku tisa

**SEOUL**, KOREA KUSINI

WACHIMBAJI migodi wawili ambao walitumia siku tisa wakiwa wamenasa chini ya ardhi katika mgodi wa zinki ulioporomoka wa Korea Kusini, wameokolewa baada ya kuishi kwa kula unga wa kahawa.

Wanaume hao, wenye umri wa miaka 62 na 56, wanaaminika wakiwa ndani ya mgodi huo, waliwasha moto na kujenga hema la plastiki.

Hata hivyo, inaelezwa wametoka ndani ya mgodi wakiwa na hali nzuri.

Wakati hayo yakiripotiwa, nchi hiyo inaomboleza baada ya zaidi ya watu 150 kufa katika mkasa kama huo katika mji mkuu Seoul wiki iliyopita.

Wachimbaji hao wawili walikwama karibu mita 200 sawa na futi 650 chini ya ardhi baada ya sehemu ya mgodi wa zinki waliokuwa wakifanya kazi kuporomoka tangu Oktoba 26, katika eneo la Bonghwa.

Juhudi za kuwaokoa zilifanikiwa juzi zaidi ya siku tisa tangu wakwame chini ya ardhi.

Wote wawili waliweza kutoka nje ya mgodi na kupelekwa katika hospitali ya mji. Daktari wao alisema watapata nafuu zaidi hivi karibuni.

Rais Yoon Suk-yeol aliita uokoaji wao kuwa wa ajabu. "Asante na asante tena kwa kurejea salama kutoka kwenye njia panda ya maisha na kifo," aliandika kwenye Facebook.

Mamlaka ilisema wachimbaji hao walinusurika kwa kunywa maji ambayo yalianguka kutoka kwenye dari na kutumia unga wa kuchanganya kahawa kama mlo.

Shughuli ya uokoaji ilianza siku ya Alhamisi wakati wafanyakazi wa dharura walipotoboa shimo na kuingiza kamera ndogo katika juhudi za kuwatafuta wachimba migodi hao, kulingana na shirika la habari la Yonhap la Korea Kusini.

Hatimaye waligunduliwa wakiwa wamekaa pamoja ili kupata joto, katika chumba kikubwa ambapo mashimo kadhaa ya migodi hukutana.

**BBC**

**SAFU**

**MAKALA**

# WINGI WETU NDIYO NGUVU YETU



Na Magabilo Masambu

OKTOBA 31, 2022 Rais Samia Suluhu Hassan alizindua matokeo ya sensa ya watu na makazi katika sherehe zilizofanyika kwenye uwanja wa Jamhuri, Dodoma. Katika uzinduzi huo, Rais alitangaza idadi ya watanzania kuwa ni 61,741,120 wanaume wakiwa 30,053,130 na wanawake 31,687,990.

Baada ya tangazo hilo, nimepata kuzungumza na baadhi ya Watanzania, ambao wametoa maoni tofauti. Wako wanaoona kwamba, idadi hiyo ni kubwa kulinganisha na hali ya uchumi wetu. Wengine wanaona bado tungali wachache na kwamba tunazo rasilimali nyingi kwa ajili ya kujenga uchumi wetu.

Lakini hivi Tanzania ni kitu gani? Ni nchi yenye eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 947,303 ikijumuisha sehemu ya nchi kavu na majini kwa maana ya bahari, maziwa na mito. Miongoni mwa nchi zilizomo katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, ukiitoa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Tanzania ndiyo nchi pekee kubwa kuliko zote, kwa mujibu wa vitabu na machapisho mbalimbali yanayobainisha ukubwa wake katika ukanda huu wa Afrika Mashariki.

Sehemu ya eneo la ardhi linatumika katika shughuli za kilimo na ufugaji, japo halijatumiwa ipasavyo katika shughuli hasa za kiuchumi, hivyo Tanzania bado inalo eneo kubwa la kutosha kwa ajili ya wananchi wake zaidi ya milioni 60 sasa. Upande wa maziwa na mito kuachilia mbali maji kutumika katika shughuli za majumbani, pia hutumika katika shughuli za uvuvi. Maziwa kama Victoria, Nyasa, Tanganyika, Manyara na mengine, hutumika kwa shughuli hizo.

Tanzania ni nchi yenye vivutio mbalimbali, zikiwamo hifadhi za taifa, ambazo ziko takribani 16 ambazo ni Arusha, Gombe, Katavi, Kilimanjaro, Mahale, Mikumi, Manyara, Ruaha, Rubondo, Serengeti, Saadani, Tarangire, Udzungwa, Kitulo, Mkomazi na Saanane. Hiiv ni kwa mujibu wa jarida la Tanzania Unforgettable. Hii yote ni upekee iliyo nao Tanzania.

Tanzania ni nchi pekee katika bara Afrika yenye mlima mrefu kuliko yote mlima mrefu kuliko yote duniani uliosimama kwa kujitegemea - Mlima Kilimanjaro, ambao una urefu wa mita 5,895 kutoka usawa wa bahari. Mbali na mlima huu, kuna milima mingine na mabonde ya kutosha pamoja na nyanda za juu kusini ambazo zinapendeza machoni mwa wageni na wenyeji.

Changamoto tulio nayo ni kwa namna gani hizi rasilimali tunaweza kuzigeuza kwa urahisi ziwe mali na tuzitumie katika kujenga nchi lakini na kuboresha maisha ya mtu mmoja mmoja. Suala si kuwa na rasilimali nyingi kisha kuzitaja na kujisifu kwamba tuna hiki na kile.

Ni muhimu sana kuweka mipango thabiti yenye kufanya mageuzi ya kiuchumi kuboresha maisha ya Watanzania zaidi ya milioni 60 sasa. Kuwa na madini, milima, mabonde mazuri ya kilimo, mbuga ni jambo moja lakini kuzibadilisha hizo rasilimali ziwe fedha ndilo tatizo. Hili ni sawa na mwanafunzi aliyenunuliwa kila aina ya kitabu nyumbani lakini darasani anakuwa wa mwisho. Kila akikutana na wenzake anawatambia jinsi alivyo na nukuu nyingi za madaftari ya kaka zake na vitabu alivyonunuliwa na baba yake lakini anashindwa kuvitumia kufaulu mitihani yake.

Kwa upande wa uhusiano wetu ya kijamii, idadi hii ya watu bado haiwezi kuwa tatizo. Watu wengine huko duniani wanajivunia wingi wao il mradi tu wingi huo unawafanya wawe wamoja zaidi kuliko kugawanyika. Tanzania tunaishi bila kujali makabila au dini zetu ndiyo mana mtu wa jamii yoyote kutoka kabila lolote anaweza kuoa au kuolewa na mtu wa kabila lolote au dini yoyote bila shida. Hii ni tofauti na baadhi ya watu katika nchi zingine ambao kabila au dini huwa ni kigezo kinachoweza kuzingatiwa wakati wa kuoa au kuolewa.

Tukitumia wingi wetu kuimarisha umoja wetu, tukatumia rasilimali zetu kama nilivyozitaja hapo juu, serikali ikatumia idadi hii kupanga mipango yake, tunaweza kuwa taifa kubwa zaidi lenye nguvu ya kiuchumi kama rasilimali hizo zitatumika kuleta maendeleo ya wananchi wote wa nchi hii.

Kwa maana nyingine, wingi wetu usije ukatumika kuvuruga nchi badala yake tuijenge. Ni kweli kwamba wakati mwingine wingi unaweza kuzaa changamoto nyingi ikiwamo ukosefu wa ajira. Kama serikali itaweka miundombinu wezeshi katika eneo la ardhi, Watanzania wakalima na kupata chakula cha kutosha, kelele za ajira zitakuwa chache na tunaweza tusijidharau.

*0689157789*
*magabilomjalifu@gmail.com*
*DAR ES SALAAM-TANZANIA*

**BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO**

# Chidumule na tofauti ya mapenzi ya pesa na pesa kwenye mapenzi



Na Adam Fungamwango

**Ni kwamba Cosmas alimpenda msichana mmoja aitwaye Cecilia. Lakini kuna jamaa mmoja mwenye pesa zake ambaye alimpenda pia, badala ya kwenda na sera zake, yeye akaenda kumponda mwanaume mwenzake kwa sababu ni fukara.**

KWENYE jamii huwa kunazuka mijadala mbalimbali huhusu pesa na mapenzi. Wakati mwingine inahamishiwa mpaka kwenye mitandao ya kijamii, baadhi wakisema pesa ndiyo kila kitu kwenye mapenzi.

Kundi hili la kwanza linasema bila pesa hakuna mapenzi. Na mtu akiwa na pesa basi anaweza kupata mpenzi yoyote yule anayemtaka na hatokuwa na tatizo lolote. Kwa maana hiyo hataathirika au kuumia kwenye kitu kinachoitwa mapenzi. Kudi hilo linaamini kuwa pesa ndiyo kila kitu. Ukiwa nazo utampata yoyote yule na mahali popote pale.

Kundi la pili linapinga na kusema pesa si kila kitu kwenye mapenzi. Hili linakubali kuwa kwa dunia ya sasa pesa ina umuhimu, lakini wanachosema ni kwamba kwanza yaanze mapenzi, halafu pesa inafanya kazi ya kurutubisha.

Watu wa kundi hili, hawaamini kuwa pesa ndiyo iwe msingi wa penzi, badala yake mapenzi yaanze ndipo pesa ifuate.

Aidha, kundi hili la pili linaamini kuwa pesa inaweza kumfanya mwanamume akapata mwanamke yoyote anayemtaka, lakini watakuwa naye kwa sababu hiyo na si penzi kutoka moyoni. Hapo pesa ikipungua humwoni mtu.

Wale ambao penzi lao linajengwa na msingi wa kukubaliana, watazitumia kwa ajili ya kutatua shida na matatizo yao yatakayowakabili na si vinginevyo. Hakuna mtu anayeweza kumwacha mpenzi wake akapatwa matatizo asimsaidie. Hapo ndipo pesa zitatumika.

Wengine wakaenda mbali zaidi na kusema mwenye pesa anaweza kununua furaha ya muda, lakini si mapenzi ya kutoka ndani ya moyo. Kwa hawa hawa wanaume wenye pesa, baadhi yao huwa na tabia ya kujikweza zaidi kutokana na uwezo wao kitu ambacho kinawakera mno kinadada.

Kinadada wao wanachotaka kusikia ni kusifiwa wao zaidi na si kukutana na mwanaume ambaye anakaa kujisifia yeye tu.

Baadhi ya wanawaume hawa pia wana tabia ya kuwaponda wenzao wasio na pesa, au wale ambao wanaonekana kuwafuata wanawake wanaowataka wao.

Wanaamini kuwa pesa yake ndiyo kila kitu, na wale wasio nazo hawastahili kupendwa. Hushangaa mwanamke anayempenda mtu mwenye pesa za wastani na badala ya kumpenda yeye. Hapo sasa ndipo kashfa zitaanza.

Simulizi hii yote inabebwa na kibao cha DDC Mlimani Park Orchestra kilichopigwa mwanzoni mwa miaka ya 1980, utunzi wake mwanamuziki Cosmas Thobias Chidumule ambaye kwa sasa anaimba njimbo za Injili.

Kwenye wimbo huu ameweka tofauti kati ya mapenzi na pesa. Ingawa zinahitajiana, lakini kwa wakati husika.

Ni kwamba Cosmas alimpenda msichana mmoja aitwaye Cecilia. Lakini kuna jamaa mmoja mwenye pesa zake ambaye alimpenda pia, badala ya kwenda na sera zake, yeye akaenda kumponda mwanaume mwenzake kwa sababu ni fukara.

Kwa bahati nzuri msichana alionekana kumpenda zaidi Cosmas badala ya jamaa mwenye pesa, hivyo akahadithiwa kila kitu.

Hakukubali, akaamua kumfuata jamaa na kumpasha ukweli juu ya jambo alilolifanya kwa msichana yule halikuwa la kiungwana. Wimbo unaitwa 'Usitumie Pesa kama Fimbo'

"Sikusimuliwa hayo ninayoyasema, nimekusikia mwenyewe ukimsimamga yule msichana. Eti kwanini amempenda mtu kama Chidumule, kwanza sina gari wala nyumba, nitampa nini huyo bibi jamani ee."

Nadhani kwa kutaka asionekana kama ameambiwa na msichana, akamwambia wala hakusimuliwa, ila amemsikia mwenyewe, akaendelea kumpa vipande vyake.

"Ameshasema hakutaki kaa chonjo, ameshasema hakutaki kaa chonjo. Lazima katika mapenzi kamwe hakuna na penzi la pesa duniani halipo, kwani hata kobe ana mpenzi wake na kamwe hajui pesa oo baba ninasema. Unamponda yule kijana ili bibi akuthamini wewe. Ukimpenda msichana sema naye polepole, kwani hakuna haja ya kumkashifu kijana mwezio oo baba."

Ni kweli kabisa penzi halilazimishwi hata kama ukiwa na mabilioni mangapi ya shilingi, yaana kwanza kwa makubaliano, vitu vingine vinafuata baadaye.

"Ameshasema hakutaki kaa chonjo, ameshasema hakutaki kaa chonjo.

Usitumie pesa kama fimbo kaka, mambo ya pesa mpaka makubaliano, hapo ndipo pesa huwa na thamani."

Hapa sasa ndiyo tunaona kuwa pesa inakuwa na thamani pale kunapokuwa na ridhaa au makubaliano. Yaani penzi tayari limeshachukua nafasi yake. Siyo kulazimisha kupendwa kwa sababu ya pesa.

"Ikiwa mapenzi mpaka bibi akupende, hata kama fundi wa kuhonga lakini mpaka bibi akubali."

Hata kama una cheo au pesa basi inabidi ukumbuke kama unataka mapenzi ya kweli ni mpaka mwanamke akupende nasi kutumia ukubwa wako.

"Cecy amesema Cosmas mpaka kufa, nami nasema Cecy wangu wa kufa na kuzikana, kipenzi changu mama. Hata njiwa ana mpenzi wake kwenye tundu ee, ingawa njiwa hajui noti wala shilingi."

Mtunzi anawakumbusha binadamu kuwa waangalie hata wanyama na ndege nao wanapendana ingawa wao hawajui noti wala shilingi. Hii ni kuonyesha kuwa hata kabla binadamu hawajatengeneza pesa mapenzi yalikuwapo.

Pesa imekuta mapenzi duniani na imechukua nafasi yake. Ni sawa kwa sababu hutumika wakati ya matatizo na faraja pia, lakini lazima watu watofautishe kati ya mapenzi ya pesa, na pesa kwenye mapenzi. Mapenzi ya pesa ndiyo yale ya hatari, msingi wake ikiwa mmoja anachohitaji ni hizo tu kama hazipo nalo halipo. Pesa kwenye mapenzi ni kuwa inatumika kurutubisha kama mbolea kwenye shamba.

*Tuma meseji 0716 350534*

**HADITHI**

# HADITHI

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaj, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele.
Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

# Harusi imevunjika-4

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Enhee babu kuna nini, maana umeniita ujue, na mimi nimekuja kwa ajili yako tu."

"Sikiliza mjukuu wangu, haya ni maisha. Kwetu sisi mila yetu inaruhusu kabisa kuhusu hili nitakalokwambia." Mzee Mbegu alisema na kusikiliza kama ataulizwa swali, lakini Jerry akawa kama amepigwa na butwaa. Hakujua ni kitu gani tena kinataka kufanyika.

Mdomo wake ulishindwa kuuliza chochote, zaidi kwa mbali alihisi woga kumuingia. Anafahamu mila mbalimbali za makabila nchini. Hata yeye kabila lake lina utamaduni na mila zake. Nyingine ni nzuri na zimeendelezwa hadi leo kwa sababu zinaweka misingi ya kuheshimiana, kujaliana, kusaidiana na kuleta upendo na umoja.

Zipo mila ambazo si nzuri, zilizopitwa na wakati ambazo watu wa makabila yale yale pamoja na serikali wamekuwa wakizipiga vita kwa sababu zinakinzana na ustawi wa jamii ya sasa iliyoendelea.

"Kwa sababu umetoa barua, ikajibiwa, ukatoa na mahari, kila mtu anakutambua hapa na tumekuwa pamoja mpaka siku ya sherehe za harusi mambo yakaharibika. Maumivu uliyoyasikia na sisi kama wanandugu upande wa mke, tumeona tufanye kitu kimoja. Tumekutafutia mke mwingine."

Pamoja na kwamba woga ulimtoka Jerry, lakini alishtuka kwani hakutegemea kuambiwa kitu kama kile.

"Mke mwingine?" Akarudia maneno ya mzee Mbegu.

"Ndiyo, tumeamua tukupe mke mwingine badala ya Vayajo. Naye ni Zulfa, ndogo wake Vayajo."

Bado Jerry alikuwa kwenye mshangao. Ni kitu kizito na cha ghafla sana alichoambiwa.

"Mdogo wake?" Akarudia tena kuuliza.

"Ndiyo, baada ya Vayajo, akafuata Jumanne, halafu ndiyo Zulfa. Huyu naona atakufaa sana. Usiogope, huyu hatotulazimisha kufanya sherehe kama ile. Ile imeshafanyika. Sisi tu huku tutafanya tu hafla fupi tu ya kifamilia halafu unamchukua bila mtu yoyote kujua, watajua wakati tayari uko naye nyumbani mnaishi."

Jerry hakujua asijibu nini kama kuna wakati alitaka kuuliza "Kama Vajayo akirudi na kukuta hiki itakuwaje?" Lakini aliona litakuwa ni swali la ajabu na la kipuuzi. Mtu aliyemkimbia siku ya harusi leo tena awe na nguvu ya kuuliza swali kama lile.




**"Huyu ndiye atakuwa mbadala kwa sababu kila kitu umeshakifanya, na huyo bibie kama akija sidhani kama ana haki tena ya kuuliza kitu ambacho amekiharibu mwenyewe."**

"Huyu ndiye atakuwa mbadala kwa sababu kila kitu umeshakifanya, na huyo bibie kama akija sidhani kama ana haki tena ya kuuliza kitu ambacho amekiharibu mwenyewe." Maneno hayo yalikuwa kama ni jibu ya kile ambacho alikuwa Jerry anawaza.

Bado Jerry aliendelea kuwaza. Kwanza hamfahamu vizuri Zulfa. Ni msichana ambaye alianza kumfahamu hivi karibuni tu, hasa kwenye maandalizi ya harusi. Na aliwahi kuambiwa kuwa kama unamhitaji msichana kuwa naye, au kumuoa ni lazima kwanza uzoeane naye. Hiyo itafanya kuanza kufahamu baadhi ya tabia zake ambazo zitakuonyesha kuwa kama unaweza ukazimudu au la. Akaambiwa ni hatari kuwa na mwanamke ambaye tabia zake unakwenda kuzikuta ukiwa tayari uko naye ndani.

"Babu, huyu Zulfa mbona mimi simfahamu vizuri, itakuwaje?"

"Ni kweli mjukuu wangu, Zulfa nusu ya maisha yake alikuwa akiishi Morogoro, kule alichukuliwa na shangazi yake. Shangazi yake alizaa mtoto mmoja tu wa kike. Sasa kwa sababu hakubahatika tena kupata mtoto akamuomba kaka yake amchukue Zulfa akaishi kama mtoto wake kwa ajili ya kumuondolea upweke. Na unaweza kuuliza kwa nini Zulfa na si Vayajo, ni kwa sababu rika lao lilikuwa moja." Ni kama vile alikuwa njia panda. Nusu alitaka kukubali, lakini bado kuna kitu kilikuwa kinamwambia akatae.

Ukimya wake wa kushindwa kukubali au kukataa ulimfanya mzee Mbegu kudhani kuwa amekubali.

"Zulfaaa" Aliita kwa sauti kavu, nene iliyoonyesha kuwa haikwenda umbali mrefu. Ni kama msichana huyo alikuwa anasikiliza kitu tangu mwanzo.

"Bee babu." Sauti ilisikika ikiitikia.

"Njoo mjukuu wangu."

Sekunde chache kabla ya kutimia nusu dakika, mlango ulifunguliwa. Aliingia msichana mmoja mwembamba, mrefu. Sura yake ilionyesha kabisa kuwa bado mbichi. Mbichi kwa maana halisi. Kwa mbali Jerry alivyoangalia sura yake ilifanana sana na Vayajo. Tofauti ni kwamba dada mtu alikuwa mweupe zaidi kuliko mdogo wake. Mwili ulijaa zaidi kuliko mdogo wake. Kitu alichovutiwa nacho zaidi ni ngozi yake ilionekana ni halisi na haina chembe ya vipodozi, pia umri wake wa miaka 22 uliifanya ngozi kumetameta kama nyoka aina ya kobra.

"Mjukuu wangu kama nilivyokwambia huko nyuma, dada yako ametuvua nguo, sasa wa kutuokoa ni wewe. Huyu bwana bado anataka mke. Tunataka wewe uchukue nafasi ya dada yako."

"Nani mimi?" Akauliza kwa sauti ndogo yenye haya, huku hata sura yake akiiweka pembeni, akiwa hataki kumuangalia mtu yoyote kati yao wawili. "Babu, mbona mimi nilidhani mnafanya utani kumbe kweli?"

Pamoja na kwamba Jerry hakuwa anaafiki moja kwa moja suala la kupewa mke, lakini jibu hilo likamshtua kidogo.

"Na akili yako unadhani sisi tulivyokwambia tulikuwa tunatania?"

"Samahani sana babu, lakini mimi siwezi."

"Kwa nini wakati tulishayaongea haya?" "Kwanza mimi sikudhani kama mlikuwa siriasi kiasi hiki, pia babu huyu si wa dada Vayajo, atanifikiriaje akisikia hili? Halafu mimi wazo la kuolewa nilikuwa hata sina, iweje ghafla hivi? Bila hata kujiandaa?"

Kukawa kimya kidogo ndani mle. Binti alijibu maswali yote ya msingi kwa ufasaha, uhakika bila hasira, kwa makini na aibu ya kike kiasi cha kumshangaza Jerry. Na hapo ndipo alipoanza kumwangalia kwa makini mno. Alimuangalia hadi mwenyewe akajua kuwa anaangaliwa kwa namna tofauti na ilivyokuwa mwanzo.

Hadi wakati huo Jerry hakuwa ameongea kitu chochote kile. Kwa sababu kwanza hadi anafika hapo hakuwa anajua ameitiwa nini. Na bado mpaka sasa alikuwa anatafakari jambo hilo na hajapata maamuzi kichwani mwake. Hata hivyo alichokasirika moyoni mwake ni kuona mambo yanajirudia. Vayajo alimtoroka siku ya harusi. Aliapa hatokwenda tena kule. Mzee Mbegu amemwita na baada ya tafakari ya kina akaamua kwenda. Anakutaka tena na kitu kama hicho.

Binti anakataa tena mbele yake. Hilo pia lilimkumbushia machungu aliyoyapata siku alipotaka kufunga ndoa.

"Nimeitwa tena kutiwa aibu? Kwa nini wasingekuwa na uhakika na hili ndiyo waniite?" Ni swali ambalo angeuliza kama isingekuwa ni heshima ya sehemu ile ambayo yeye aliichukulia kama ukweni.

"Mimi nadhani hakijaharibika kitu. Nadhani niwaachie tu mjadala uendelee na chochote kikiwa tayari mtaniambia. Kama shemeji ataendelea na msimamo sawa, na kama hatoendelea nayo si vibaya ni uamuzi wake na wala msimlazimishe. Nadhani sasa wewe nenda kapumzike." Jerry alimaliza utata huo kwa hekima, hakutaka malumbano au majibizano ambayo yangeleta sintofahamu.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# ANJELLA NDO BASI TENA KONDE GANG

MWIMBAJI nyota wa Bongofleva Harmonize, amepasua jipu na kubainisha kwamba msanii wa kike aliyekuwa akimsimamia, Anjellah, kwa sasa yupo huru kufanya kazi na watu wengine.

Harmonize ambaye anatamba na album mpya ya "Made for us" amefunguka hayo kupitia ukurasa wake wa Instagram kwa kueleza kwamba mtu yeyote anayetaka kuendeleza kipaji cha Anjella, basi asisite kujitokeza.

Mwanamuziki huyo hakuweka wazi kwenye posti hiyo kama Konde Gang wameachana rasmi na Anjella, lakini kauli yake hiyo inaonyesha msanii huyo ameondolewa katika lebo hiyo.

"Nimejitahidi kadri ya uwezo wangu najua kuna wenye uwezo mkubwa kunizidi ukizingatia nimeanza juzi, kama kuna anayeweza kumuendeleza kipaji chake ni faraja kwangu na asisite kujitokeza," amesema Harmonize

# SERIKALI KUWAKUTANISHA WASANII AFRIKA

**Na Pili Kigome**

WIZARA ya Utamaduni, Sanaa na michezo imedhamiria kuinua sekta ya sanaa nchini kwa kuwaunganisha wasanii wa Tanzania na wenzao wa Afrika ili kuweza kukuza uwezo na ufanisi wa kazi zao.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dkt. Hassan Abas alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa mikutano wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere.

Abas aliviambia vyombo vya habari kuwa wameandaa tamasha kuwakutanisha wanamuziki wa bara la Afrika litakalofanyika nchini.

Alisema tamasha hilo linatarajiwa kuanza Novemba 24 hadi 26 mwaka huu litawapa fursa wanamuziki wa Tanzania kukutana na wanamuziki wengine wa ngazi ya kimataifa kuweza kubadilishana ujuzi na kukua kibiashara.

Akizungumza katika mkutano huo Katibu Mkuu wa shirikisho la wasanii msanii Faridi Kubanda (FidQ) aliwataka wasanii wajitokeze kujiandikisha bila gharama yoyote kwani ni faida kwao kukutanishwa na wanamuziki wa ngazi ya kimataifa.

HABARI MICHEZO

### BELLINGHAM SAFI LIVERPOOL
KLABU ya Liverpool wanapigiwa upatu kuzishinda Chelsea, Manchester United, Manchester City na Real Madrid katika usajili wa Jude Bellingham kutoka Borussia Dortmund baada ya kujenga uhusiano wa karibu na kiungo huyo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 19. ***(ESPN)***

### ZAHA HATASUMBUKA
KOCHA wa Crystal Palace, Patrick Vieira amesema uvumi wa uhamisho hautamsumbua fowadi wa Ivory Coast, Wilfried Zaha. Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 unamalizika msimu wa joto. ***(Press Association via Mail)***

### MARTINEZ KUMRITHI PIQUE
BARCELONA wanapanga kusajili beki mpya wa kati Januari kuchukua nafasi ya Gerard Pique aliyestaafu, huku mlinzi wa Hispania na Athletic Bilbao, Inigo Martinez mwenye umri wa miaka 31, akiwa anaongoza kwenye orodha yao. ***(Mundo Deportivo)***

### SILVA KUTUA BARCA
KUSTAAFU kwa Gerard Pique pia kutaipatia Barcelona fedha za kumnunua kiungo wa kati wa Manchester City na Ureno, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 28. ***(Sport)***

### COSTA ATAKIWA MAN
KLABU ya Manchester United wamemfuatilia mlinda mlango wa Porto na Ureno Diogo Costa mwenye umri wa miaka 23, mara kadhaa msimu huu huku kocha Erik ten Hag akimuwania kwa udi na uvumba. ***(90 Minutes)***

### BEEK KUBAKI MAN
KOCHA wa Manchester United, Erik Ten Hag hana nia ya kumuweka kando kiungo wa Uholanzi, Donny van de Beek, akisema anajua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 anaweza kufanya vyema zaidi. ***(Mirror)***

### TIELEMANS HAONDOKI JANUARI
KIUNGO wa kati wa Leicester City na Ubelgiji, Youri Tielemans, ambaye amekuwa akihusishwa sana na Arsenal na Newcastle United, hana uwezekano wa kuruhusiwa kuondoka Januari, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 anaweza kuwa huru mkataba wake utakapokamilika mwisho wa msimu. ***(Leicester Mercury)***

### SKRINIAR KUBAKIZWA INTER
KLABU ya Inter Milan wanajitahidi kutaka kumbakiza mlinzi wa Slovakia, Milan Skriniar baada ya kubainika kuwa timu kubwa za Ligi Kuu ya England ziko tayari kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(90 Min)***

### LASCELLES KUUZWA
KLABU ya Newcastle United itapokea ofa ya kumuuza beki wa England, Jamaal Lascelles mwenye umri wa miaka 28. ***(Football Insider)***

### ALMIRON ALIWINDWA
MANCHESTER United, Arsenal na Southampton zote zilionyesha nia ya kumsajili Miguel Almiron aliye katika kiwango bora kabla ya kiungo huyo wa Paraguay mwenye umri wa miaka 28 kuamua kujiunga na Newcastle United mwaka wa 2019. ***(ABC Cardinal via Manchester Evening News)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DEPAY: SIJAKATAA KUREJEA UWANJANI

Ni baada ya kudaiwa kuwa anaogopa akirudi anaweza akaumia na kukosa kombe la Dunia..

**BARCELONA, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Memphis Depay amekanusha madai kuwa amekataa kurejea uwanjani licha ya kupona jeraha lake ili kujilinda kabla ya Kombe la Dunia.

Memphis alipata jeraha la msuli wa paja Septemba na hajaichezea klabu yake katika mechi kumi zilizopita za mashindano yote.

Ripoti kutoka Hispania zimedai kwamba, Mholanzi huyo anachelewesha kurejea kwake uwanjani kwa makusudi ili kuhakikisha hapati matatizo kabla ya Kombe la Dunia.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, Memphis amezungumzia uvumi huo na kusema: "Kusikia uvumi fulani usio na heshima kunihusu hakupunguzi kasi ya jeraha langu.

"Vyombo vya habari vinashiriki mambo kwa urahisi bila kujua ukweli ambao matokeo yake huzua simulizi hasi kuzunguka jina langu!"

Huko nyuma wakati Memphis alipopata jeraha, ambalo lilikuja katika mchezo wa ligi ya mataifa ya Uefa dhidi ya Poland katika ngazi ya kimataifa, vyombo vya habari vya Uholanzi viliripoti kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 angepatikana tena ndani ya 'wiki nne au tano'.

Huku ikiwa haijawekwa tarehe ya kurejea, Barcelona wanasemekana kukubali kwamba Memphis hatashiriki katika klabu yake kabla ya Kombe la Dunia, ambalo litaanza takribani wiki tatu zijazo.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
CHELSEA
VERSUS
ARSENAL
1 | 2.58
X | 3.28
2 | 2.58

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# XAVI AZIPA KOMBE LA DUNIA ARGENTINA, BRAZIL



**BARCELONA, Hispania**

XAVI anaamini kuwa Lionel Messi hatimaye anaweza kutwaa Kombe la Dunia nchini Qatar mwaka huu, akionesha Argentina pamoja na Brazil kama ndio timu zinazopewa nafasi kubwa ya kutwaa taji hilo.

Messi alikaribia kuwa mshindi wa Kombe la Dunia wakati Argentina ilipofungwa na Ujerumani kwenye fainali ya mwaka 2014.

Mafanikio yake ya kubeba mara saba tuzo ya Ballon d'Or yanadhihirisha ukuu wa Messi, lakini anakosa tuzo ya timu ya taifa inayothaminiwa kuliko zote.

Kushinda taji la Copa America akiwa na Argentina mwaka jana kulimpa taji kubwa la kwanza katika soka la kimataifa la wakubwa, huku Argentina ikiishinda Brazil katika fainali pale kwenye dimba la Maracana.

Sasa, akiwa na umri wa miaka 35, na katika Kombe lake la mwisho la Dunia, nahodha wa Argentina, Messi anaweza kulitwaa, kwa mujibu mchezaji mwenzake wa zamani wa Barcelona, Xavi.

"Argentina na Brazil ziko hatua mbele ya timu zote," alisema Xavi.

"Ninaona wana nguvu sana kama timu, pia na wachezaji binafsi, wa kimwili na kwa mbinu na mikakati pia, ni timu mbili kubwa.

"Nadhani wako hatua mbele ya baadhi ya timu bora za Ulaya hivi sasa. Lakini katika Kombe la Dunia huwezi kujua. Kila kitu kinaweza kuwa kigumu."

Xavi, mshindi wa Kombe la Dunia mwaka 2010 akiwa na Hispania na sasa kocha mkuu wa Barcelona, aliongeza: "Timu za Ulaya ni muhimu sana: Hispania, Ufaransa, hata England, wana timu zenye nguvu, lakini nadhani Brazil na Argentina wako mbele zaidi."

Brazil ni mabingwa mara tano wa Kombe la Dunia, lakini hawajashinda tangu mabao nane ya Ronaldo yaliwafanya walibebe taji hilo mwaka 2002, huku Argentina wakiwa wamebeba taji hilo mara mbili, 1978 na 1986.

# Barcelona yaongeza nguvu kumtwaa Silva

**MANCHESTER, England**

BARCELONA imeripotiwa kurejea katika mbio zao za kumtaka kiungo wa Manchester City, Bernardo Silva, na inasemekana wana uhakika na uwezo wao wa kukamilisha dili hilo Januari.

Silva mwenye umri wa miaka 28, ameshinda mataji manne ya ligi Kuu England akiwa na City tangu alipowasili katika klabu hiyo mwaka wa 2017, na anafurahia msimu mwingine mzuri.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno aliyeichezea nchi yake mechi 72 ana mabao mawili na asisti tano katika mechi 12 za ligi msimu huu, na ameonekana katika mechi zote sita za City za hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.




Barcelona wamekuwa wakihusishwa na Silva kwa miezi kadhaa na sasa wanaonekana kuwa na nafasi kubwa ya kumsajili januari.

Kwa mujibu wa Sport, kustaafu kwa Gerard Pique kumesababisha kuimarika kwa hali ya kifedha kwa Barcelona, na kuwaruhusu kurejea tena nia yao ya muda mrefu ya kumnunua Silva.

Ripoti hiyo inadai kuwa City wanaweza kusitasita kuachana na mchezaji huyo, lakini Silva aliomba hapo awali kuondoka klabuni hapo.

Wakati huo huo, Mundo Deportivo inaongeza kuwa Barcelona watamtazama mlinzi wa kati wa Athletic Bilbao, Inigo Martinez mwenye umri wa miaka 31 kama chaguo lao la kuziba pengo la safu ya ulinzi iliyoachwa na Pique.

Y | CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 06/11/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:15 | 5625 | Utrecht vs Groningen | 1.67 | 3.82 | 4.57 |
| 14:30 | 1053 | Gaziantep BB vs Kayserispor | 2.21 | 3.39 | 3.04 |
| 14:30 | 1887 | Bologna vs Torino | 2.91 | 3.06 | 2.44 |
| 15:00 | 1183 | Chelsea vs Arsenal | 2.58 | 3.28 | 2.58 |
| 15:00 | 1642 | St Johnstone vs Rangers | 9.74 | 5.37 | 1.27 |
| 15:00 | 5912 | Lorient vs Paris St Germain | 8.36 | 5.46 | 1.30 |
| 15:30 | 2925 | KAA Gent vs Brugge | 2.68 | 3.38 | 2.46 |
| 16:00 | 3296 | Atletico Madrid vs Espanyol | 1.44 | 4.21 | 7.21 |
| 16:30 | 3020 | FC Volendam vs Feyenoord | 6.55 | 5.36 | 1.35 |
| 16:30 | 5101 | Twente vs GO Ahead Eagles | 1.35 | 4.86 | 7.54 |
| 17:00 | 1124 | Monza vs Verona | 2.14 | 3.37 | 3.17 |
| 17:00 | 1762 | Sampdoria vs Fiorentina | 3.81 | 3.37 | 1.92 |
| 17:00 | 2304 | Aston Villa vs Manchester Utd | 3.17 | 3.30 | 2.17 |
| 17:00 | 2673 | Antalyaspor vs Fatih Karagumruk | 1.96 | 3.47 | 3.62 |
| 17:00 | 3141 | Southampton vs Newcastle | 3.81 | 3.51 | 1.88 |
| 17:00 | 4305 | Toulouse vs Monaco | 3.04 | 3.69 | 2.10 |
| 17:00 | 4504 | Clermont Foot vs Montpellier | 2.35 | 3.44 | 2.79 |
| 17:00 | 4605 | Reims vs Nantes | 2.04 | 3.43 | 3.43 |
| 17:00 | 4726 | Nice vs Brest | 1.81 | 3.59 | 4.09 |
| 17:00 | 5098 | West Ham vs Crystal Palace | 1.87 | 3.41 | 3.96 |
| 17:30 | 1628 | Bayer Leverkusen vs Union Berlin | 2.10 | 3.36 | 3.27 |
| 18:00 | 5033 | Hearts vs Motherwell | 1.93 | 3.55 | 3.65 |
| 18:15 | 2137 | Real Sociedad vs Valencia | 1.92 | 3.35 | 4.00 |
| 18:15 | 4211 | Real Oviedo vs Granada | 2.45 | 2.93 | 3.03 |
| 18:30 | 1058 | Rio Ave vs Boavista | 2.38 | 3.08 | 3.03 |
| 18:30 | 1976 | FC Lugano vs FC Zurich | 2.22 | 3.33 | 3.08 |
| 18:30 | 2716 | FC Basel vs FC Sion | 1.77 | 3.79 | 4.09 |
| 18:45 | 4766 | Waalwick vs AZ Alkmaar | 3.86 | 3.86 | 1.78 |
| 18:45 | 4961 | Ajax vs PSV Eindhoven | 1.72 | 4.06 | 3.96 |
| 19:00 | 3767 | Rapid Vienna vs LASK Linz | 2.32 | 3.31 | 2.73 |
| 19:00 | 3977 | Rostov vs Dinamo Moscow | 2.57 | 3.41 | 2.52 |
| 19:05 | 2646 | Lille vs Rennes | 2.41 | 3.48 | 2.68 |
| 19:10 | 3972 | Dinamo Zagreb vs HNK Sibenik | 1.14 | 6.59 | 13.57 |
| 19:30 | 4555 | Tottenham vs Liverpool | 3.13 | 3.53 | 2.10 |
| 19:30 | 4790 | SC Freiburg vs FC Koln | 1.67 | 3.86 | 4.46 |
| 20:00 | 1385 | Roma vs Lazio | 1.96 | 3.46 | 3.56 |
| 20:00 | 2293 | Trabzonspor vs Konyaspor | 1.89 | 3.39 | 3.99 |
| 20:30 | 1337 | Royal Antwerp vs Anderlecht | 2.20 | 3.33 | 3.13 |
| 20:30 | 3639 | Panathinaikos vs Olympiakos | 2.20 | 3.18 | 3.28 |
| 20:30 | 3727 | Villarreal vs Mallorca | 1.59 | 3.84 | 5.59 |
| 21:00 | 2328 | Maritimo vs Famalicao | 2.69 | 3.14 | 2.59 |
| 21:00 | 4909 | Sporting Braga vs Casa Pia Atletico | 1.39 | 4.68 | 6.97 |
| 21:30 | 4511 | Beitar Jerusalem vs Maccabi Haifa | 8.38 | 5.07 | 1.28 |
| 21:30 | 4627 | Asteras Tripolis vs AEK Athens | 5.18 | 3.44 | 1.69 |
| 22:45 | 4033 | Juventus vs Inter | 2.92 | 3.27 | 2.32 |
| 22:45 | 5874 | Marseille vs Lyon | 2.17 | 3.49 | 3.04 |
| 23:00 | 5143 | Oostende vs Kortrijk | 2.13 | 3.49 | 3.14 |
| 23:00 | 5378 | Albacete Balompie vs Levante | 2.45 | 3.08 | 2.88 |
| 23:00 | 5563 | Betis vs Sevilla FC | 2.15 | 3.21 | 3.41 |
| 23:30 | 4662 | GD Estoril vs Benfica | 8.97 | 5.38 | 1.29 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SERIKALI YAJIPANGA KUTAFUTA KOCHA TIMU YA TAIFA

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Mohammed Mchengerwa amesema kulingana na mwenendo mbaya wa timu za Taifa hasa kwa wanaume wako katika mpango mkakati wa kutafuta makocha kutoka nje ya nchi.

Akizungumza katika hafla ya ufunguzi wa mafunzo kwa walimu wa michezo kutoka shule teuliwa 56 nchini Tanzania iliyoandaliwa na Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Mchengerwa alisema kuna matatizo makubwa katika timu za taifa ndio maana serikali imeamua kuwekeza katika mchezo huo.

Alisema hatua iliyopo sasa kwa Tanzania wanabahatisha hasa kwa timu za wanaume na kupongeza timu za Wanawake ambazo zimekuwa zikifanya vizuri.

"Nina imani kutofanya vizuri kwa timu zetu hizi ni kwa sababu hatuna msingi kuanzia chini, mafunzo haya kwa walimu yatakuwa msaada mkubwa kwa serikali katika mpango mkakati wake wa kuibuka wachezaji kutoka ngazi ya shule.

"Tunakiri hatuna msingi katika michezo. Sasa hivi ndio tunaanza msingi kwa kuanza chini kwenda mashuleni kwa mpango mkakati wa miaka 8 ijayo, na mwaka 2030 Tanzania tunataka kwenda kucheza kombe la Duniani," alisema.

Tuko katika mchakato wa kutafuta kocha mkuu ambaye atalipwa na serikali kama ilivyokuwa hapo awali na kutoshirikiana na viongozi au makocha wazawa ambao kazi yao kupenyezea wachezaji ambao hawana uwezo," alisema.

Alisema BMT ijipange kwa sababu timu za Taifa ziko mikononi mwa serikali hali hiyo wanatakiwa kukutana na vyama husika katika mchakato wa kupatikana makocha wenye uwezo mkubwa na amekuwa na rekodi nzuri katika michezo husika.

"Walimu mliokuwa katika mafuzo mnatakiwa kujiongeza huko katika shule mnazofundisha na kutosubiri fedha za serikali zitoke kwa ajili ya vifaa bali wanatakiwa kuanza kwa kufanya jogging na mazoezi mengine huku wakisubiri fedha za Serikali."

Alisema mbali na kuwepo kwa shule 56, wako katika mchakato wa kupata fedha zingine kwa ajili ya kuongeza shule mbili jumla kuwe na idadi ya 58.



Baadhi ya wanafunzi wa Shule mbalimbali za Msingi na Sekondari mkoani Dar es Salaam wakifanya mazoezi ya mpira wa magongo katika viwanja vya Jakaya Kikwete Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Simba makucha

INATOKA UK. 24

kiasi kwamba wanakuwa roho juu kama hakuwa sehemu ya kikosi. Timu hiyo ipo kwenye nafasi ya pili ya msimamo ikiwa na pointi 17, huku Singida Big Stars ikiwa nafasi ya sita, ikikusanya pointi 14.

## Yanga SC yatua

INATOKA UK. 24

pungufu yao ili waondoke na ushindi katika mchezo huo.


"Mchezo wa ugenini mara nyingi unakuwa na mipango zaidi tofauti na ukiwa nyumbani wachezaji wanapaswa kujitoa mara mbili ya nyumbani kwani kupata ushindi kwenye ardhi ya ugenini ni ngumu,"

Mashindano ya ZFF, mchezo huo umesogo

# Michezo

Jumapili Novemba 6, 2022

Nipashe

**Depay: Sijakataa kurejea uwanjani**

UKURASA 21



Wachezaji wa Yanga, Jesus Moloko (kushoto) na Bakari Mwamnyeto wakiwa wamepumzika baada ya kuwasili jijini Tunis wakijiandaa na safari ya kuelekea mji wa Sousse. **PICHA: YANGA**

# Yanga SC yatua kibabe Tunisia

Kujifua siku mbili mji wa Sousse kabla ya kuwavaa Club Africain jijini Tunis...

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Yanga juzi kiliwasili salama katika mji wa Sousse nchini Tunisia kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa marudiano wa kombe la Shirikisho Barani Afrika dhidi ya Club Africain, ambapo itaweka kambi ya siku mbili.

Katika mchezo wa kwanza timu hizo zilitoka suluhu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, hivyo Yanga inahitaji ushindi au sare ya mabao ili iweze kutinga hatua ya makundi.

Yanga wamepata pigo kwenye mchezo huo kwani watamkosa mlinzi wake wa kulia, Djuma Shabaan ambaye anasumbuliwa na msuli wa nyama ya paja ambao aliumia kwenye mchezo wa mkondo wa kwanza.

Akizungumza na gazeti hili kutoka Tunisia kocha msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze alisema licha ya kukosekana kwake, lakini haitaathiri mipango yao kwani wachezaji wa kuziba nafasi yake wapo.

Alisema watamkosa Djuma na hiyo haitabadilisha mipango yao kwa sababu ya uwepo wa nyota wengine, huku Kibwana Shomari akitarajiwa kuziba nafasi yake.

"Tutaingia kwenye mchezo huu tukiwa na lengo moja la kutafuta ushindi wapinzani wetu katika mchezo wa kwanza walikuwa wanazuia zaidi, lakini nafikiri watakuja kivingine kwani timu itakayoshinda inaenda makundi," alisema Kaze.

Alisema wanajua ugumu wa mchezo huo wamejifunza kutokana na makosa ya mchezo uliopita wanaendelea kuyafanyia ma-

INAENDELEA UK. 23

# Simba makucha yote kwa Singida Big Stars

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Simba kilichoanza Jumanne iliyopita rasmi mazoezi kwenye Uwanja wa Mo Arena, Bunju, Dar es Salaam, kiliingia kambini jana kwa ajili ya kujiwinda dhidi ya Singida Big Stars, huku kiungo wake mkabaji, Sadio Kanoute akirejea.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Selemani Matola amesema kikosi kilianza mazoezi ya asubuhi kwa siku tatu huku wakirejea nyumbani, na baada ya hapo kikosi kimeingia rasmi kambini na kuanza mazoezi ya asubuhi na jioni.

"Wachezaji waanza kambi baada ya mazoezi ya siku tatu asubuhi tu huku wachezaji wakirejea makwao, kambi inaanza kwa ajili ya mechi ijayo, furaha iliyokuwepo hata waliokuwepo majeruhi nao wamerejea, kama Sadio Kanoute naye ameanza mazoezi, mategemeo wiki hii kabla ya mechi ya Singida kikosi chote kitakuwa kiko imara kamili kwa ajili ya mechi hiyo.

Simba imeanza mazoezi baada ya kucheza mechi ya Ligi Kuu mara ya mwisho Jumapili iliyopita, ikiibandika Mtibwa Sugar mabao 5-0, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Timu hiyo inatarajia kucheza dhidi ya Singida Big Stars Jumatano ijayo kwenye Uwanja wa Liti, mkoani Singida ikiwa ni mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu, timu zote zikienda kucheza raundi ya tisa.

Kurejea kwa Kanoute ambaye mashabiki wa timu hiyo wamempachika jina la 'Putin', kunaonekana kuwa faraja kwa wanachama na mashabiki kwani wamekuwa na imani naye sana anapocheza kwenye nafasi ya kiungo wa kukaba.

Pengo lake lilionekana kuiathiri timu hiyo ilipocheza dhidi ya Azam FC Oktoba 27 na kupoteza kwa bao 1-0.

Kanoute raia wa Mali amekuwa mhimili wa timu hiyo hasa msimu huu ambapo kiwango chake kimepanda na kuwakosha mashabiki wa timu hiyo

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >